Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

... Na kama Mwenyezi Mungu Asingaliwazuia watu, baadhi yao kwa wengine, bila shaka yangalivunjwa mahekalu na makanisa, na nyumba za ibada na misikiti ambamo jina la Mwenyezi Mungu hutajwa kwa wingi...
(Al-Hajj 22:41)

JUZU 73 No. 170 | DHUL-HIJJA 1433 AH | NOVEMBER 2012 | NUBUWWAT 1391 HS | BEI TSH. 500/=

Kiongozi wa Ahmadiyya duniani ahutubia seneti ya Marekani na kusema:

Njia ya kuhakikisha amani – Uhusiano wa haki baina ya mataifa

Na Mussa Mpinga,
Dar es Salaam

Hotuba iliyotolewa na Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a., Khalifatul Masih V, Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya, katika Ukumbi wa Capitol Hill Marekani, Juni 2012



Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya duniani (mwenye kilemba) akisindikizwa na maseneta wa Marekani kutoka ukumbini baada ya kuwahutubia

Bismillahi – Rahmanir – Raheem.

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehema, mwingi wa Ukarimu.

Waheshimiwa Wageni wote – Assalaam Alaikum wa rahmatullah wabarakaatuh/ - Amani na rehema za Allah ziwe juu yenu wote.

Kabla sijaendelea, napenda kwanza kabisa kuchukua fursa hii kuwashukuruni wote kwa kutumia muda huu kuja ili kusikiliza ninachotaka kusema. Nimeombwa kuzungumzia juu ya mada yenye eneo pana sana na yenye kuhusisha mambo mengi. Ina vipengele vingi mbalimbali, kwa hiyo, haiwezekani kwangu kuvipitia vyote katika muda mfupi uliopo. Mada niliyotakiwa kuiongelea ni upatikanaji wa amani duniani. Kwa hakika hili ni jambo la muhimu sana na ni dharura inayoikabili dunia leo. Hata hivyo kwa kuwa muda ni mfupi, nitatoa kwa kifupi tu maoni ya Islam juu ya kuleta amani kupitia uhusiano wa haki na usawa baina ya mataifa.

Ukweli ni kwamba amani na haki havitenganishiki – huwezi ukawa na kimoja bila ya kingine. Kwa hakika kanuni hii ni kitu ambacho watu wote wenye busara na akili wanakielewa. Ukiacha wale ambao wamekusudia

Endelea uk. 3

(TEHAMA) Rehema ya Ushindi wa Islam

Hotuba iliyotolewa kwenye Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) Tanzania, iliyofanyika Kitonga, Dar es Salaam tarehe 29-9-2012

Na Jamil Mwanga,
Dar es Salaam

Tukiwa katika zama hizi za teknolojia ya kisasa, mtu anaweza kujiuliza swali kwamba maendeleo haya yote ya teknolojia yanatufanya tujikite kwenye utajiri wa mali na fedha? Je, mabadiliko haya yanatupeleka mbali na Mwenyezi Mungu? Au je, ni ya kishetani?

Kwa hakika haya ndiyo maswali ambayo mara nyingi watu hujiuliza. Lakini tunatakiwa tufikiri kuhusu muda au kipindi ambacho mabadiliko haya yanatokea. Ni kwa nini yanatokea wakati wa zama za Masihi Aliyeahidiwa (a.s)?

Mabadiliko haya makubwa yanatokea kipindi hiki ambacho amedhihiri Masihi Aliyeahidiwa (a.s), hivyo, swali kubwa tunalojiuliza ni kwamba: Je, tunaweza kuziita zama hizi za kielektroniki kuwa ni zama za Masihi Aliyeahidiwa (a.s)? Zama za maendeleo ya Jumuiya ya Ahmadiyya?

Mwenyezi Mungu anatuambia ndani ya Qur'an Tukufu kuwa: "Na kama Tukikuondoa, basi sisi tutajilipiza kisasi kwao" (43:42).

Hii inaonyesha kuwa ahadi yoyote anayotoa Mwenyezi Mungu dhidi ya maadui wa mitume, hutimia barabara, iwe ni wakati wa uhai wa nabii, au baadaye. Vivyo hivyo, baadhi ya habari njema hutimia wakati wa uhai wake ilhali habari nyingine hutambulika baadaye.

Wakati Mtume Mtukufu (s.a.w.) alipoeleza habari njema kuhusu [Dola ya Iran], Suraka, ilimaanisha ushindi wa Islamu huko Persia. Hii ilitokea wakati wa Ukhalifa wa Hadhrat Umar (radhi ya Allah iwe juu yake).

Hivyo, ili kuweza kupata jawabu la swali hili tunalojiuliza, ni lazima turudi nyuma katika Bara Arabu, wakati wa zama za Hadhrat Muhammad (s.aw) wakati Allah alipomwambia ndani ya Qur'an Tukufu (5:4):

"Leo nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islamu iwe dini yenu."(5:4)

Endelea uk. 4

Jalsa Salana 2012 yapata mafanikio zaidi

Na Mwl. Maliki Mbawala
Kitonga, Dar es Salaam

Kama ilivyo kawaida ya Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya duniani kote, Jamaat Ahmadiyya Tanzania ilifanikiwa kufanya Jalsa Salana yake (Mkutano wa mwaka) wa 43 kuanzia tarehe 28/9/2012 hadi 30/9/2012, Kitonga nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam. Miongoni mwa vitu vilivyopamba Jalsa hiyo ni kukamilika kwa kiasi kikubwa kwa ujenzi wa ukumbi wa mkutano sehemu ya akinababa. Pia ujenzi wa madarasa ya shule ya Sekondari ya Ahmadiyya Kitonga na kumalizika kwa ofisi ya Lajna Imaillah kuliongeza uzuri katika mandhari ya mkutano wa mwaka huu.

Ujenzi wa ukumbi wa mkutano ulianza mwezi Julai 2012, hivyo kukamilika kwake kwa kiasi cha kuweza kutumika kunaonesha msaada wa Mwenyezi Mungu juu ya Jumuiya hii, kwani maandalizi hayo yalikuwa kwa njia ya kujitolea kwa hali na mali kwa wanajumuiya.

Katika uwanja huu wa kujitolea, Waqar Amal mbalimbali ziliandaliwa kwa kuwashirikisha Khuddam, Lajna na Ansarullah ili

Endelea uk. 2

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

TATIZO KUBWA

Tatizo kubwa linalomkabili binadamu hivi leo, sio umasikini kwani Allah Ametupa rasilimali za kutosha ili zitumike kwa faida yetu sisi sote. Wala tatizo letu sio vita, kwani Allah Ametupa hekima na busara ya kumaliza matatizo yetu kwa amani na salama. Tatizo kubwa linalotukabili ni kuendelea kuwa na kiu wakati tuko ziwani! Tatizo kubwa kupita yote ni kwa dunia kutotambua taa inayotoa mwanga mbora wa viumbe wote, sababu ya kuumbwa dunia, rehema kwa ulimwengu wote, bwana wa daraja na mfano bora kwa binadamu wote Mtukufu Mtume Muhammad amani na rehema za Mwenyezi Mungu ziwe kwake.

Ni dhuluma kubwa na ukatili wa hali ya juu kumnasibisha Mtukufu Mtume Muhammad (saw) na aina yoyote ya umwagaji wa damu, uonevu na uhasama. Maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni kitabu kilicho wazi na ufafanuzi bayana ulitolewa na mama wa waaminio alipoulizwa juu ya maisha ya Mtume (saw) naye akasema mwenendo wake ni Qur'an Tukufu.

Hakuna Nabii ambaye maisha yake yameelezwa kinagaubaga kama ya Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Alikuwa yatima, akafanya biashara, akaingizwa vitani, akawa mfalme, na kila alichokigusa kiligeuka kuwa lulu ya thamani. Fikiria safari yake ya Taif alipopigwa hadi damu ikachuruzika na malaika wakamuuliza tufanye nini kwa watu hawa wa Taif, akasema wasamehewe kwani vizazi vyao vitagundua haki. Bwana mmoja alipanga kumuua Mtume Mtukufu Muhammad (saw) Seyidna Umar (ra) akamleta kwa Mtume (saw) na akaeleza yote aliyokuwa amepanga kuyafanya. Suala la kwanza aliloulizwa; Je amekula? Seyidna Umar (ra) alichoka. Kwa sauti za 'Takbir' Mtume Mtukufu (saw) aliingia mji wa Makka na akawasamehe wote ambao kwa miaka 13 walimtesa.

Mateka wa vita aliposikia sauti zao za maumivu aliamuru wapunguziwe maumivu yao. Wakristo walikuja Madina akafanya nao mazungumzo na katika Msikiti wake Mtukufu akawaruhusu waendeshe ibada yao. Aliwasaidia akina mama katika kazi za ndani, alishona viatu vyake, alikesha usiku akiomba hadi miguu yake ikavimba. Kila jambo lake alililifanya kwa ajili ya Allah. Alianza kula kwa kumkumbuka Allah, alivaa nguo mpya na akamkumbuka Allah. Alipoingia Msikitini akamkumbuka Allah. Huyo ndiyo Mbora wa viumbe wote ambaye kwa bahati mbaya sana hivi leo anadharauliwa.

Sisi tunayo huruma kubwa kwa viumbe wa Mwenyezi Mungu, tungependa wanyooke na wafuate njia iliyonyooka. Hivyo tunatoa wito kwa binadamu wote kuwaheshimu viongozi wa wa dini nyingine. Watu wanaopendwa na kuheshimiwa na watu wengine tuna haki gani ya kuwatukana na kuwabeza?

Sisi Waislam tunao wajibu mkubwa wa kuonesha mfano ambao tunajifunza kutoka kwa Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Binadamu anathamini zaidi vitendo kuliko maneno. Tueneze sifa ya Islam na utukufu wa Mtume (saw) kwa vitendo.

Huu ni wakati wa kuongeza kasi zetu katika kumsalia Mtukufu Mtume Muhammad (saw), wakati wote tunapotembea njiani, tukiwa kwenye mabasi, ofisini na mashambani daima tuendelee kumsalia Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ambaye ni rehema kwa ulimwengu wote.

Huu ni wakati wa kuifanya kila nafsi duniani itambue thamani na utukufu wa huyu mbora wa daraja Mtukutu Mtume Muhammad (saw) ili hatimaye kila nafsi iweze kushangaa kama alivyoshangaa Shaabani Robert katika kusadikika. "
"Moyo wa nani usiohuzunika kwa msiba kama huu", "Uko wapi uso usiotahayari kwa aibu kama hii", "Macho gani yasiyolengalenga machozi kwa ubaya huu?"

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Jalsa Salana 2012 yapata mafanikio

Kutoka uk. 1



Amir wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania Sh. Tahir Mahmood Chaudhry akihutubia kwenye Jalsa Salana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Jumuiya Bw. Seif Hassan Nakuchima akitoa tafsiri ya hotuba hiyo na kushoto ni Afisa Jalsa kwa mwkaa 2012 Bw. Mwinyimvua Ussi

kuhakikisha kwamba maeneo mbalimbali ya ujenzi na matayarisho mengine yanakamilika kwa wakati.

Juhudi mbalimbali zilifanyika na kamati ya ujenzi kuhakikisha kwamba ukumbi unakamilika sawa na mipango ilivyopangwa.

Mara kadhaa wanakamati wa kamati hii wakiongozwa na fundi mkuu mzee Athumani Kilimo iliwabidi kubaki Kitonga kwa siku kadhaa bila kurejea majumbani mwao.

Katika jumla ya mafanikio ya Jalsa salana ya mwaka huu ni idadi kubwa ya washiriki ikilinganishwa na mwaka jana, kwani mwaka huu walifikia watu 2500. Aidha wageni wa ndani na nje ya nchi walihudhuria Jalsa hiyo. Miongoni mwa wageni waliohudhuria walitokea Uingereza, Burundi, Malawi, Mozambique na Pakistan. Wageni wa ndani ya nchi waliohudhuria walitokea takriban mikoa yote nchini Tanzania bila ya kuwasahau ndugu kutoka Zanzibar (visiwa vya Unguja na Pemba).

Aidha katika mkutano huo walihuhduria viongozi mbalimbali wa Serikali akiwemo Mkuu wa Mkoa wa Simiyu Mh. Pascal Mabiti, Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala Mh. Khamis Chaurembo na Diwani wa Kata ya Msongola Mheshimiwa Angelina Adam Malembeka.

Majirani zetu waliozunguka katika uwanja wa Jalsa Gah pia nao walialikwa na kuhudhuria katika Jalsa hiyo.

Wageni wengine kadhaa walioalikwa na waliotoka nje ya Dar es Salaam ambao sio Waahmadiyya walifika katika Jalsa hii.

Kama ilivyo ada na kwa kuzingatia malengo na madhumuni ya kuanzishwa kwa Jalsa Salana, mada mbalimbali za kusisimua, kuongeza elimu na imani, zilizotolewa na wataalamu wa Jumuiya ziliupamba mkutano huo. Mada hizo zilizjikita katika nyanja mbalimbali za majukumu yetu kama wanajumuiya zikiwemo haja ya kutimiza wajibu wetu katika elimu, malezi, utii, haki za kinamama, haki za watoto pamoja na wajibu wetu wa kutumia Tehama katika kufikisha ujumbe wa Islam duniani kote.

Wanakamati wa idara mbalimbali nao walijitolea usiku na mchana kuhakikisha wageni wanahudumiwa vizuri pasi na matatizo wala shida yoyote. Kwa hakika Mwenyezi Mungu Atatoa ujira mwema sawa na juhudi walizozifanya wanakamati hao. Amin.

Usemi wangu wa mwisho ndugu wote napenda kuwakumbusha kuwa kumalizika kwa Jalsa ya 2012 ndiyo kuanza kwa maandalizi ya Jalsa ya mwakani 2013.



Sehemu ya washiriki kwenye Jalsa Salana ya mwaka 2012

Njia ya kuhakikisha amani

Kutoka uk. 1

kuleta machafuko duniani, hakuna yeyote kamwe ambaye angeweza kudai kwamba katika jamii yoyote, nchi au dunia nzima kunaweza kuwa na machafuko au ukosefu wa amani wakati haki na kustahiana kungalipo.

Pamoja na ukweli huu, tunakuta katika sehemu nyingi za dunia kwamba machafuko yanaonekana kwa ndani yaani ndani ya nchi yenyewe, na kwa nje yaani katika uhusiano baina ya nchi mbalimbali.

Machafuko na vurugu kama hizi zinakuwepo pamoja na kwamba serikali zote zinadai kuendesha siasa zake kwa msingi wa haki. Wote wanadai kwamba uletaji wa amani ndio lengo lao la awali. Lakini, bado, kwa jumla, hakuna shaka kwamba ukosefu wa utulivu na wasiwasi unaongezeka duniani, na kwa hiyo machafuko yanaenea. Hii inathibitisha bayana kwamba mahali fulani katika mstari, sharti za haki hazitimizwi.

Kwa hiyo, kuna haja ya haraka ya kujaribu kukomesha uonevu popote na wakati wowote unapokuwapo. Kwa ajili hii, nikiwa kiongozi wa Dunia nzima wa Jumuia ya Waislamu ya Ahmadiyya, ninapenda kutoa maoni machache juu ya haja ya, na njia za kufikia amani kwa misingi ya haki.

Jumuiya ya Waislamu ya Ahmadiyya ni Jumuiya inayojishughulisha na dini tu. Ni imani yetu thabiti kwamba yule Masihi na Mujaddid ambaye aliahidiwa kuja katika zama hizi na kuuangazia ulimwengu juu ya mafundisho sahihi ya Islamu tayari ameshafika. Tunaamini kwamba mwanzilishi wa Jumuiya yetu, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadiani a.s. alikuwa ndiye Masih na Mujaddid yule aliyeahidiwa, na kwa hiyo tumemkubali.

Aliwahimiza wafuasi wake kufuata na kueneza mafundisho ya kweli ya Islam ambayo msingi wake ni Quran Tukufu. Kwa hiyo kila kitu nitakachokieleza kuhusiana na uletaji wa amani, na kuhusiana na usimamishwaji wa haki katika uhusiano baina ya mataifa, yatasimamia kwenye msingi wa mafundisho ya Quran Tukufu.

Kuhusiana na upatikanaji wa amani ya dunia, ninyi nyote daima mnatoa maoni yenu, na kwa hakika mnafanya juhudi kubwa. Fahamu zenu zenye ubunifu na akili zinawawezesha kutoa hoja nzito, kupanga mipango na kwa hakika kuwa na muono wa amani. Kwa sababu hii suala hili halihitaji kwamba mimi nilizungumze kwa mtazamo wa kidunia au wa kisiasa, bali badala yake mtazamo wangu wote utakuwa juu ya jinsi ya kuleta amani kwa msingi wa dini. Kwa lengo hili kama nilivyoeleza mapema nitatoa baadhi ya miongozo ya muhimu sana kutokana na mafundisho ya Quran Tukufu.



Sehemu ya washiriki kwenye mkutano uliofanyika Capitol Hill, wakati Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akiwahutubia Maseneta na viongozi wengine wa Marekani

Ni muhimu kukumbuka daima kwamba elimu ya binadamu na akili yake sio kamilifu, bali kwa kweli ni pungufu. Hivyo wakati wa kufanya maamuzi au kujenga fikra mara nyingi mambo fulani huingia katika fahamu ya binadamu, ambayo yanaweza kutia wingu kwenye tafakari na kupelekea mtu kujaribu kukidhi haja zake binafsi. Hatimaye hii yaweza kupelekea kwenye matokeo yasiyo na haki, na uamuzi usio wa haki kufanyika. Sheria ya Mungu kwa upande mwingine ni kamilifu na kwa hiyo tamaa ya kisirisiri na upendeleo havipatikani ndani yake. Hii ni kwa sababu Mungu anataka tu hali njema na maendeleo ya viumbe vyake. Kwa hiyo sheria yake inasimama kikamilifu kwenye msingi wa haki. Siku ambayo watu wa dunia watatambua na kuelewa ukweli huu muhimu itakuwa ndio siku ambayo msingi wa amani ya kweli na ya kudumu utakuwa umewekwa. Vinginevyo, twaendelea kuona kwamba ingawaje jitihada zinafanywa bila kikomo katika kuleta amani ya dunia, bado zimeshindwa kuleta matokeo ya maana.

Baada ya kwisha kwa vita kuu ya kwanza ya dunia, viongozi wa baadhi ya nchi walipenda kuwapo kwa uhusiano mwema na wa amani kati ya mataifa yote katika siku zijazo.

Kwa hiyo, katika jitihada za kuleta amani ya dunia muungano wa mataifa (League of Nations) uliundwa. Lengo lake la msingi ilikuwa ni kulinda amani ya dunia, na kuzuia kuzuka kwa vita katika siku zijazo. Kwa bahati mbaya kanuni za muungano huo na maazimio ulioyapitisha yalikuwa na makosa mbalimbali na upungufu na kwa ajili hii hayakuweza kulinda barabara haki za watu wote na mataifa yote sawa sawa. Matokeo yake, kwa sababu ya kutokuwepo usawa kulikokuwapo, amani ya kudumu haikuweza kupatikana. Jitihada za muungano huo zilishindwa na hii ilipelekea moja kwa moja kwenye vita kuu ya Pili.

Wote tunafahamu uharibifu usiomithilika na mauwaji yaliyotokea ambapo takriban watu 75 milioni duniani walipoteza maisha yao, wengi wao wakiwa raia wasio na hatia. Vita ile ilipaswa kuwa ya kutosha na kuwezesha kuundwa sera ambazo zingetoa haki kwa pande zote, kwa misingi ya uadilifu, na hivyo kuwa njia ya kuleta amani duniani. Serikali za kidunia wakati huo zilijaribu kwa kiasi fulani kuleta amani na hivyo Umoja wa Mataifa ukaundwa (UNO). Hata hivyo, muda si mrefu ikaja kuonekana wazi kabisa kwamba lengo adhimu na muhimu lililoleta Umoja wa Mataifa halingeweza kufikiwa. Kwa hakika, leo baadhi ya nchi bila kificho zinatoa kauli za kuonyesha kwamba Umoja wa Mataifa umeshindwa kufikia lengo lake.

Islam inasema nini kuhusiana na uhusiano wa mataifa yaliyo katika msingi wa haki, na hivyo kuwa njia ya kuleta amani? Katika Qurani Tukufu, Mungu Mwenye Enzi anaweka wazi kwamba, wakati ambapo utaifa wetu na kutokana kwetu na makabila mbalimbali kunatoa nafasi ya kutambuana, tofauti hizi hazitoi haki wala ruhusa ya aina yoyote ya ubora wa baadhi ya watu juu ya wengine.

Hivyo Quran inaweka wazi kwamba watu wote wamezaliwa sawa. Zaidi ya hayo katika hotuba ya mwisho kutolewa na Mtume Mtukufu Muhammad s.a.w., aliwaelekeza Waislamu wote kukumbuka daima kwamba Mwarabu sio bora zaidi kuliko asiye Mwarabu. Alifundisha kwamba mtu mweupe sio bora kuliko mweusi na hali kadhalika mtu mweusi sio bora kuliko mweupe. Kwa hiyo, ni fundisho la wazi la Islam kwamba watu wa mataifa yote na rangi zote ni sawa. Vile vile, imewekwa bayana kwamba watu wote wanatakiwa wapewe haki sawa bila ya ubaguzi au upendeleo wa aina yoyote. Huu ndio ufunguo wa kanuni ya thamani ambayo inaweka msingi wa maelewano kati ya makundi na mataifa mbalimbali na kwa ajili ya kuleta amani.

Hata hivyo, leo tunaona kwamba kuna mgawanyiko na utengano baina ya nchi zenye nguvu na zile zilizo dhaifu. Kwa mfano, katika Umoja wa Mataifa tunakuta kwamba kuna tofauti iliyowekwa baina ya nchi mbalimbali. Hivyo, katika Baraza la Usalama kuna wanachama wa kudumu na wengine wasio wanachama wa kudumu. Mgawanyiko huu imethibitika kuwa ni sababu ya ndani ya kuleta wasiwasi na kukata tamaa na hivyo kila wakati tunasikia ripoti za nchi mbalimbali kulalamikia ubaguzi huu.

Islam inafundisha haki timilifu na usawa katika mambo yote na kwa ajili hii tunakuta mwongozo mwingine wa muhimu katika sura ya 5 aya ya 3 ya Qurani Tukufu. Katika aya hii mnasemwa kwamba ili kutimiza kikamilifu sharti za haki ni muhimu kuwatendea hata wale watu ambao huenda nje ya mipaka yote katika chuki yao na uadui, kwa uadilifu na usawa. Quran inafundisha kwamba popote na yeyote anayekushawishi uelekee kwenye mema na utawa unapaswa kukubali na popote na yeyote anapokusihi uelekee kwenye ukosefu na mwenendo wa dhuluma, wapaswa kukataa.

Swali ambalo linazuka kiasili ni kwamba ni kiwango gani cha uadilifu kinahitajika na Uislam? Katika sura ya 4 aya 136, Quran Tukufu inasema kwamba hata kama inabidi utoe ushahidi dhidi yako, au dhidi ya wazazi wako, au wapendwa wako hapo ni lazima ufanye hivyo ili kustawisha uadilifu, na ukweli. Nchi zenye nguvu na utajiri hazipaswi kupora haki za nchi maskini katika juhudi za kulinda maslahi yao, na wala wasijihusishe na nchi maskini kwa namna isiyo na uadilifu. Kwa upande mwingine, nchi maskini na dhaifu hazitakiwi kupanga kuzidhuru nchi zenye nguvu au tajiri hata nafasi ya kufanya hivyo inapojitokeza. Badala yake pande zote zapaswa kujitahidi kushikilia kikamilifu misingi ya uadilifu. Kwa hakika hili ni jambo la muhimu sana katika kulinda uhusiano wa amani baina ya mataifa.

Sharti nyingine ya amani kati ya mataifa kwa msingi wa uadilifu imetolewa katika sura ya 15 aya 89 ya Quran Tukufu ambayo inasema kwamba hakuna taifa linalotakiwa kutazama kamwe kwa matamanio kwenye raslimali na mali ya wengine. Hali kadhalika, hakuna nchi inayopaswa kujaribu kutwaa pasi na haki au kunyang'anya raslimali za nchi nyingine kwa kisingizio cha kujaribu kuisaidia au kuiunga mkono. Hivyo, kwa msingi wa kutoa msaada wa kiufundi, nchi zisijifaidishe kwa unyonge wa nchi nyingine kwa kufanya makubaliano ya biashara yasiyo ya haki au mikataba. Vivyo hivyo kwa msingi wa kutoa utalamu au msaada, nchi hazipaswi kujaribu kushika hatamu za raslimali au nyenzo za nchi zinazoendelea.

Pale ambapo watu walio na elimu ndogo au nchi zinahitaji kufundishwa jinsi ya kutumia raslimali zao, hapo jambo hili lifanyike.

Kisha mataifa na serikali zapaswa siku zote kutafuta namna ya kuwahudumia na kuwasiadia wale wenye bahati ndogo. Hata hivyo, huduma hiyo isitolewe kwa nia ya kupata faida fulani ya kitaifa au ya kisiasa au kama njia ya kutimiza tamaa za kisirisiri. Tunaona kwamba katika miongo sita au saba iliyopita Umoja wa Mataifa umeanzisha mipango

Endelea uk. 4

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Rehema ya Ushindi wa Islam

Kutoka uk. 1

Wakati ule Allah aliikamilisha dini ya Islam, na kuifanya iwe imekamilika. Hata hivyo, rasilimali hazikuwepo ili kueneza ujumbe huu wa Islam. Na hii imekuwa ni desturi ya Allah kwamba humtuma Nabii na kumpatia ujumbe. Ujumbe ule haukubaliwi na watu wengi wakati wa uhai wa Nabii. Ni wakati tu anapokuwa amefariki ndipo Allah huonyesha nguvu na kudura yake wakati wa dhihirisho la pili. Wakati wa dhihirisho la pili, husababisha ujumbe ule kuenea kwa wingi. Ndio maana Mtume Mtukufu (s.a.w) alitabiri kwamba Masihi atakuja katika siku za mwisho na shabaha ya kuja kwake ni kuhuisha Islam na kuueneza duniani kote. Wakati ule Jumuiya ya Ahmadiyya ilipokuwa na wafuasi wachache (mfano: Waumini 75 tu walihudhuria Jalsa Salana ya kwanza kule Qadiani), Allah alimwahidi Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba:
"I shall caurse thy message to reach the Corners of the earth", (Al Hakam, Sura ya II). Yaani, Nitaufikisha ujumbe wako katika kila pembe ya dunia.
Allah pia alimwambia:
"I shall give you a large party of Islam", (Brahin-i-Ahmadiyya, Sura 1, uk 664). Yaani, Nitakupatia Jumuiya kubwa ya Waislamu.

Hivyo, kama utabiri huu na ahadi hizi zilikuwa ni za kweli, Na Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amefika, Je, ingewezekanaje kwamba raslimali na vifaa vya teknolojia ya kisasa visiwepo ili kuthibitisha ukweli wa madai haya?
Tukumbuke pindi Allah anapotuambia ndani ya Qur'an Tukufu kuwa:
"Naapa kwa (pepo) zinazopelekwa kwa uanana,
Kisha zikazidisha mwendo na kuvuma kwa kasi,
Na kwa wale wenye kutawanya mtawanyo kamili,
Na kisha wanazibainisha tofauti," (77:2-5)

Naapa kwa (pepo) zinazopelekwa kwa uanana, Kisha zikazidisha mwendo na kuvuma kwa kasi maana yake ni kwamba awali mafundisho au ujumbe huenea hatua kwa hatua huku kasi yake ikiongezeka. Baadaye kudra ya Mwenyezi Mungu, husababisha mazingira mazuri ya haraka na ya zaidi kufanya kazi ya kueneza ujumbe wake. Tunatakiwa daima tukumbuke kwamba nguvu za Mwenyezi Mungu hazina kikomo. Kama akipenda anaweza kutimiza ahadi zote na ushindi wakati wa uhai wa nabii. Hata hivyo, ni kwa mapenzi yake kwamba wafuasi wa nabii nao pia washiriki katika kazi hii ili kupata baraka na ushindi.

Aidha, aya zinaendelea kufafanua kuwa Na kwa wale wenye kutawanya mtawanyo kamili inabainisha kuhusu kueneza ujumbe ule ambao Mtume Mtukufu (Saw) alikuja kuueneza. Ndiyo ujumbe kuhusu dini ya kweli ambayo itadumu hadi siku ya Kiama, na Masihi Aliyeahidiwa (a.s) amekuja katika zama hizi ili kuhuisha ujumbe huu. Mwenyezi Mungu ametoa njia za kisasa za kueneza ujumbe huu. Masahaba wa Mtume Mtukufu Saw hawakuwa na njia zozote za kisasa lakini walifanya Tabligh (mahubiri) kwa shauku. Siku hizi njia na rasilimali zipo, zilikusudiwa kwa ajili ya zama za mfuasi wake mkweli na mnyenyekevu, na aya hii (Na kwa wale wenye kutawanya mtawanyo kamili) inabashiri kuhusu suala hili.

Ndio maana leo hii tunashuhudia zama za kielekrtoniki tofauti kabisa na dunia ilivyoweza kushuhudia hapo kabla. Katika zama hizi za mtandao wa mawasiliano ya kompyuta na intaneti, suala la muda na umbali limekuwa halina maana tena. Vikwazo vimeondolewa na mipaka ya kimataifa imekuwa haina maana. Taratibu na sheria zinazotawala dunia hapa hazina nafasi na matarajio ni mengi yasiyo na kikomo.
Hebu tufikirie hali hii, hususan ambapo kizazi kilichokuwa kikifanya tafiti kwa kutumia vitabu badala ya Google/ intaneti; na kuandika kwenye karatasi (writing pad) badala ya ipad, inatufanya tupate usumbufu wa namna Fulani. Aidha, watu wengine wanasema kwamba uvumbuzi na mabadiliko haya ni uovu na husababisha hasara kubwa na yameharibu familia na nyumba zetu na yanaharibu jamii.

Leo hii, nipo hapa kuwaelezeni kwamba zama hizi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)/kielektroniki sio za kuharibu jamii na kwa hakika zimekuja ili kusambaza Islam. Zama hizi zimekuja ili kusaidia shabaha ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Zimekuja ili kuleta mabadiliko makubwa na ya msingi ya namna ya kufanya mahubiri na kuwa njia ya kuwakusanya watu pamoja chini ya Bendera ya Islam.

Allah (s.w), mjuzi wa ghaib alitoa utabiri wa mabadiliko yote haya miaka 1400 iliyopita katika Sura AT-TAKWIIR pale aliposema:
"Na nafsi zitakapounganishwa", (81:8)



Mtoa mada, Bw. Jamil Mwanga, akiwa mbele ya jukwaa wakati akitoa mada yake

Aya hii inabashiri wakati ambapo njia za usafiri zitarahisishwa sana kiasi hiki kwamba watu wa mataifa ya mbali watakusanywa pamoja. Uvumbuzi wa gari moshi, ndege na magari kwa hakika ulitabiriwa kupitia aya hii ya Qur'an Tukufu.

Njia za kisasa za usafiri zimeondoa au kupunguza umbali na usumbufu na zimefanya watu wakutane. (Rejea mkusanyiko wa Jalsa Salana UK, Canada, Marekani,

Endelea uk. 5

Njia ya kuhakikisha amani

Kutoka uk. 3

mingi na taasisi mbalimbali kwa lengo la kusaidia nchi maskini kupata maendeleo. Katika juhudi hizi wametumia raslimali za nchi zinazoendelea. Hata hivyo, pamoja na juhudi hizi zote, hakuna nchi yoyote inayoendelea ambayo imefikia kwenye hatua au kiwango cha nchi zinazoendelea. Moja wapo ya sababu ya hili bila shaka ni ufisadi ulioenea katika nyingi ya serikali za nchi hizo zenye maendeleo haba. Kwa masikitiko hata hivyo, ni lazima niseme kwamba pamoja na haya, kama njia ya kuendeleza maslahi yao, nchi zilizoendelea zimeendelea kushirikiana na nchi kama hizi. Mipango ya biashara, misaada ya kimataifa na mikataba ya biashara imeendelea kuchakatwa. Matokeo yake, mfadhaiko na kukosekana utulivu kwa maskini na makundi ya wasionacho katika jamii yameendelea kuongezeka na hii imepelekea kutokea kwa uhaini na machafuko ndani ya nchi hizo. Watu maskini wa nchi zinazoendelea wamefikia hatua ya kukata tamaa kiasi hiki kwamba wamegeuka sio tu dhidi ya viongozi wao, bali pia dhidi ya mataifa makubwa vile vile. Hali hii inayanufaisha makundi yenye msimamo mkali, ambao wametumia fursa ya fadhaa hiyo na hivyo wameweza kuwahimiza watu kama hao kujiunga na makundi yao na kuunga mkono falsafa yao iliyojaa chuki. Hatimaye matokeo yake yamekuwa kwamba amani ya dunia imeharibiwa.
Hivyo Islam imezielekeza fikra zetu kwenye njia mbalimbali za kuleta amani. Inataka uadilifu kamili. Inataka ushahidi wa ukweli daima utolewe. Inataka kwamba macho yetu yasielekezwe kwa matamanio kwenye mali za wengine. Inataka kwamba nchi zilizoendelea ziweke kando tamaa zao za kisirisiri na badala yake ziwasaidie na kuwahudumia wenye maendeleo duni na nchi maskini, kwa mtazamo na nia ya kujitolea kwa kweli.
Ikiwa mambo haya yote yataangaliwa, basi hapo amani ya kweli itapatikana.
Ikiwa pamoja na hatua zote hizi zilizotajwa hapo juu, nchi yoyote inavuka mipaka yote na kuishambulia nchi nyingine, na ikataka bila haki kuchukua umiliki wa raslimali zake, hapo nchi nyingine ni lazima zichukue hatua ya kuzuia ukatili kama huo. Lakini wapaswa daima kutenda hivyo kwa uadilifu.
Mazingira ya kuchukua hatua kwa kufuata mafundisho ya Islam yameelezwa katika Quran, katika sura ya 45. Inafundisha kwamba pale mataifa mawili yanapokuwa katika mgogoro na huo ukapelekea kwenye vita, hapo nchi nyingine zinapaswa kuwaasa kwa bidii sana warejee kwenye mazungumzo na majadiliano ili waweze kufikia maelewano na makubaliano kwa msingi wa upatanishi. Ikiwa pamoja na hayo, moja ya pande hasimu hairidhii hadidu za mapatano na unaanzisha vita, hapo nchi nyingine zinapaswa kuungana ili kumzuia mvamizi yule. Nchi vamizi inaposhindwa na kukubali majadiliano, hapo pande zote zapaswa kujielekeza nguvu zao kwenye mapatano ambayo yanaleta amani na maelewano ya kudumu. Masharti magumu na yasiyo ya haki hayapaswi kuwekwa ambayo hupelekea mikono ya taifa lolote kufungika, kwa kuwa katika muda mrefu hilo litapelekea kutokuwepo utulivu hali ambayo itachemka na kuenea. Matokeo ya kukosekana huku kwa utulivu ni machafuko zaidi.
Katika mazingira ambayo nchi ya tatu inajaribu kupatanisha nchi mbili hasimu, hapa inapaswa kufanya hivyo kwa uaminifu na bila ya upendeleo wowote. Inatakiwa kusiwe na upendeleo wowote hata kama nchi moja wapo itaisema vibaya nchi patanishi. Kwa hiyo, nchi ya tatu inatakiwa kutoonyesha hasira katika hali kama hiyo. Haitakiwi kujaribu kulipiza kisasi, wala haipaswi kuacha kufuata adili. Pande zote zinatakiwa zipewe haki zake.
Hivyo kwa sharti za uadilifu kutimizwa, ni muhimu kwamba nchi patanishi zenyewe zisijaribu kutafuta maslahi yao, wala kujaribu kujinufaisha kinyume cha haki kutoka kwa nchi moja wapo. Haipaswi kuingilia bila haki au kuishinikiza yoyote ya pande husika kwa dhuluma. Raslimali za nchi zisinyakuliwe. Vikwazo visivyo vya lazima wala vya haki visiwekwe kwenye nchi hizi kwa sababu hiyo si haki wala kufanya hivyo hakuwezi kuwa sababu ya kuboreka kwa uhusiano baina ya nchi.
Kwa sababu ya ufinyu wa muda, nimejaribu tu kwa kifupi kutaja nukta hizi. Kwa kifupi kama tunataka amani ipatikane duniani, basi ni lazima tuweke kando maslahi yetu binafsi na maslahi ya kitaifa kwa ajili ya hali njema iliyo pana zaidi na pia ni lazima tujenge maelewano baina yetu kwa msingi wa haki.
Vinginevyo, baadhi yenu mtakubaliana nami kwamba kwa sababu ya mashirikiano, makundi makubwa yataundwa siku zijazo au naweza kusema yameanza kuundwa – na si kama haielekei kwamba machafuko yataendelea kuongezeka duniani, ambayo hatimae yatapelekea kwenye uharibifu mkubwa. Matokeo ya machafuko kama hayo na vita bila shaka yatadumu kwa vizazi vingi.
Kwa hiyo, Marekani kama nchi yenye nguvu zaidi duniani, yapaswa kutimiza wajibu wake kwa kuenenda kwa uadilifu na kwa nia njema kulingana na nilivyoeleza. Ikiwa itafanya hivyo basi dunia daima itaikumbuka kwa upendo juhudi yenu kubwa. Ni maombi yangu (kwa Mungu) kwamba itokee hivyo. Ahsanteni sana. Ahasanteni tena.
Sawa na desturi yetu mwishoni mwa shughuli kwa kawaida tunafanya maombi ya kimya. Hivyo nitafanya maombi ya kimya na Waahmadiyya wakinifuata. Ninyi nyote wageni wetu mwaweza kuomba kwa namna yenu.

Mwisho.

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Rehema ya Ushindi wa Islam

Kutoka uk. 4

Tanzania n.k).

Kama vile hiyo haitoshi, tunatakiwa pia tutafakari kuhusu zama hizi. Marshal McLuhan, Profesa katika Chuo Kikuu cha Toronto aliibua usemi usemao: "Global village" yaani: "Dunia kama kijiji" akijaribu kuelezea dunia mpya baada ya maendeleo makubwa ya Vyombo vya upashanaji Habari (televisheni, redio, magazeti) pamoja na intaneti. Hii inamaanisha kwamba kuishi katika zama za kielektroniki, inaonekana kana kwamba dunia imekuwa kijiji kimoja ambapo kila mmoja na kila kitu kinaweza kupatikana kiganjani.
Vizuizi vyote vya zamani vimeondolewa. Watu hukutanishwa kwa njia ya mtandao/kielekroniki kwa sekunde. Ukiwa Tanzania unaweza kuzungumza na mtu yeyote duniani kupitia Skype au MSN kwa sekunde, inakuwa kana kwamba mmekaa kwenye chumba kimoja mkifurahia kwa pamoja.

Katika Sura hiyo hiyo ya Qur'an Tukufu, Allah anaendelea kusema:
"Na sahifa zitakapoenezwa", (81:11)
Akielezea aya hii, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) anaandika:
"Tazameni vipo viwanda vingapi vya uchapishaji nchini India na katika nchi nyingine. Huu ni mpango ya Allah (s.w) ili atusaidie katika kazi yetu na hivyo kueneza dini yetu, vitabu vyetu na uelewa wetu miongoni mwa watu wa duniani ili waweze kusikiliza kile tunachokisema na wapate kuongoka". (Ainah Kamalate Islam).

Hadhrat Khalifatul Masih IV rh aliandika zaidi kuwa:
"Njia kubwa na yenye nguvu ya kuwaunganisha watu ni kupitia uchapishwaji wa vitabu, magazeti, majarida n.k. njia zote za usafiri zimechangia katika kuwaunganisha watu duniani, lakini mchango/dhima ya Vyombo vya Habari kamwe hauwezi kupuuzwa au kuwa na mbadala wa njia nyingine yoyote ya kuunganisha watu. Fikiria jukumu kubwa la kusambaza vitabu katika maeneo mbalimbali katika zama hizi, licha ya umbali kufupishwa, ghafla umbali ule unawezakuongezekatena. Watu watakuwa wametenganishwa. Ni katika mazingira haya ya kisasa ya upashanaji habari na uchapishwaji wa vitabu kwa wingi unaotajwa katika aya hii." (Revelation, Rationality, knowledge and Truth, uk, 598-599).

Kama mabadiliko haya yasingalikuwepo, Je, ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ungewezaje kuenezwa? Leo hii kwa kutafuta ukitumia mtandao wa intaneti kama Google, kila mmoja anaweza kupata vitabu na maandiko yake kwa muda mfupi sana wa si zaidi ya sekunde.

Sasa swali muhimu sana ni kwamba, ikiwa vifaa na raslimali zote hizi zimepatikana, kila kifaa kipo kwa ajili yetu, Je, ni yapi majukumu yetu?

Khalifa Mtukufu V a.t.b.a anatukumbusha kuwa:
"Zama za Masihi Aliyeahidiwa (a.s) ni zama za kueneza vitabu. Ametuachia hazina ya vitabu vyake. Hivi vitabu/maandishi yake yalichapishwa wakati wa uhai wake na masahaba wake walifanya kazi kubwa ya kuvieneza. Waliifanya kazi hii kwa njia ya kujitolea kama ilivyokuwa wakati wa zama za mwanzo za Islamu wakati wa Masahaba wa Mtume Mtukufu (S.a.w). Wafuasi wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) pia wapo karibu na Mwenyezi Mungu. Siku hizi, Mwenyezi Mungu amejaalia njia za kueneza vitabu hivi na kuwajibu wapinzani, njia ambazo ni za haraka na zenye uwezo kuliko hapo kabla. Qur'an Tukufu na vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (a.s) na vitabu vingine vinaoneshwa kwa njia ya matangazo ya televisheni na intaneti". Alhamdulillah, hata baadhi ya vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa (a.s) vilivyotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili sasa vinapatikana kwenye intaneti kupitia google au kwenye tovuti ya Jamaat ya 'www.alislam.org'.

Siku hizi kila mfanyakazi wa televisheni ya MTA, bila kujali mahali anakofanyia kazi duniani, kwa hakika wao wanafanya kazi ya kufikisha ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) katika kona za dunia. Mwenyezi Mungu atatimiza jambo hili. Yeye alimfunulia Masihi Aliyeahidiwa (a.s) kwamba kuhusu kufikisha ujumbe huu katika kila kona za dunia', na kwa ajili hii Amejaalia kuwepo kwa rasilimali hizi za teknolojia ya kisasa. Jambo hili limekusudiwa, na ushahidi ni mabadiliko yote (ya teknolojia) yanayotokea. Kama tutatimiza wajibu wetu kwa kushiriki katika Tabligh tutakuwa wenye kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu, na kuendelea kutafakari suala hili, tutakuwa kweli tunatimiza wajibu wetu. Ikumbukwe kuwa televisheni ya MTA inafanya kazi chini ya mwongozo na uangalizi wa Khalifatul Masih wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya. Miaka 1400 iliyopita Mtume Mtukufu (S.a.w) alitabiri pia kuhusu vifaa na teknolojia hizi za kisasa kwamba: Siku moja kila neno litapatikana kupitia sauti ya mwanadamu na ujumbe utasafirishwa umbali mrefu na kuenea kote duniani. Hebu tufikiri kama wale waliokuwepo wakati wa zama za Mtukufu Mtume (S.aw) wangeona leo hii baadhi ya teknolojia hizi za kisasa, wangalishtuka kwamba mawe na vyuma vinaweza kuzungumza na kufikisha ujumbe wa Allah! Hivyo, tukitazama mashine hizi, vifaa na uvumbuzi wa teknolojia za kisasa inaonekana kama miujiza kwamba sio tu zimekuja ili kutoa mawasiliano na elimu pekee bali kuuhamasisha ubongo wa mwanadamu. Lengo ni kuwezesha mafundisho bora ya Qur'an Tukufu kumfikia kila mtu, kila nyumba leo na katika zama hizi kama Allah alivyoahidi na ndio kwa utukufu na Baraka hizi za MTA suala hili linatimia. Mwanzoni MTA ilikuwa ikipatikana kwa saa 5 tu kila siku huko Ulaya na sasa tangu mwaka 1996 imekuwa ya kimataifa (MTA International) ikirusha matangazo yake duniani kote kwa saa 24 kwa kutokana na michango ya fedha zinazochangwa na wanajumuiya wenyewe. Vipindi huandaliwa kutoka sehemu mbalimbali duniani na mara nyingi hutolewa kwa lugha tofauti kupitia chaneli za sauti (mathalani, Kiurdu, Kijerumani, Kiarabu, Kibengali, Kifaransa, Kituruki, Kiindonesia, Kiswahili n.k). inarusha matangazo yake moja kwa moja kote duniani kwa lugha takribani nane kwa wakati mmoja huku pia vipindi vyake vikijikita na kuzingatia tofauti ya mazingira na tamaduni za nchi mbalimbali duniani. Vipindi pia huhusisha dini, Taarifa za Habari, michezo, sayansi, utabibu, kujifunza lugha, vipindi vya watoto n.k Hata wakati wa Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) huu wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya kule Uingereza iliripotiwa kuwa mwaka huu wakati wa Mkutano wa mwaka idadi ya watu waliokuwa wakipokea na kutazama moja kwa moja matangazo ya MTA kupitia mtandao wa intaneti wa www.mta.tv iliongezeka na kufikia takribani laki tatu.

Mtume Mtukufu (S.a.w) amesema: "Nendeni mkatafute elimu hata kama mtatakiwa kwenda Uchina." Hili lilikuwa tamko zito mnamo karne ya 6 huko Uarabuni kwa sababu inaonyesha ni jinsi gani tunavyotakiwa kuwa na kiu ya kutafuta elimu. Lakini hivi sasa, huduma hii imesogezwa, kwamba Allah ameileta dunia yote-kwa njia ya mtandao wa kompyuta. Mtandao huo ukiwa umejazwa elimu na tunaweza kuipata viganjani, tukiwa majumbani na mara kadhaa tunashindwa kunufaika nayo kwa kisingizio cha shughuli nyingi.

Kwa kuwa maendeleo haya ya teknolojia kwa kiasi fulani ni mapya, na wengi wetu hatuna uelewa nayo. Kimsingi hii inafanya hususan wazazi au walezi kuwa makini. Mara kwa mara tunawasikia wazazi/ walezi wakionesha wasiwasi wao kwa watoto wao wadogo ambao hutumia muda mwingi kwenye intaneti au michezo ya kompyuta maarufu kama "game". Wao hutaka watoto wao waachane na komyuta. Hata hivyo, siku hizi bila kujali mahali tulipo, watoto watakwenda kwenye mtandao wa mawasiliano ya kompyuta. Jambo la msingi ni kuwafunza vyema ili waweze kutumia vizuri muda wao. (mfano Mtoto ana simu ya mkononi ambapo anaweza kupata intaneti na huwezi kumzuia)-

Ndugu zangu, hebu tufikirie zama za Mtume Mtukufu (S.a.w). Fikiria wale akina mama ambao walikuwa wakiwatuma watoto wao kujifunza ujuzi wa kivita. Ni watoto hao wadogo ambao baadaye walikufa mashahidi na wakawa chanzo cha nuru ya Islam.

Leo hii, Allah (s.w) ametutwika jukumu hili mabegani mwetu. Tunawajibika kwa ajili ya kizazi hiki na vizazi vijavyo. Tofauti pekee iliyopo ni kwamba siku hizi badala ya kuwafundisha watoto wetu ustadi wa upanga, tunatakiwa tuwafundishe matumizi ya inteneti, Vyombo vya Habari na njia zingine za kisasa za kielektroniki. Je, tupo tayari kubeba jukumu hili?

Tukirejea ndani ya Qur'an Tukufu, Allah (s.w) anatuambia:
"Je, huoni kwamba Mwenyezi Mungu Ameziumba mbingu na ardhi kwa haki? Kama akipenda atawaondoeni na kuleta viumbe wapya. Na hilo kwa Mwenyezi Mungu si gumu." (14:20-21)

Hivyo, kama hatuko tayari kueneza ujumbe wa Mwenyezi Mungu, basi Allah atatuondoa na kuleta watu wengine ambao watakuwa na shauku ya kueneza ujumbe Wake. Sitarajii kwamba baada ya kusikiliza mwito huu, yeyote miongoni mwetu atataka kubaki nyuma. Huu ndio wakati, hivyo chonde chonde tuamke na tutekeleze majukumu yetu.

Allah anasema katika Qur'an Tukufu kwamba:
'Kataba Llahu La-a-^Libana ana warusululiy', yaani Mwenyezi Mungu amekwisha andika kuwa Bila shaka "Nitashinda Mimi na Mitume wangu!" (58:22).
Hivyo, kama tukiangalia zama za Mtume Mtukufu (s.aw), ingawaje makafiri walitumia zana nzito za kivita kama upanga, ngao, farasi na ngamia ili kuangusha Islam, historia ni shahidi kwamba waislamu walitumia zana kama hizo ambazo zilikuwa hazitoshelezi na hatimaye walipata ushindi.

Historia inajirudia leo hii. Hizi ni zama za Ushindi wa Islam Ahmadiyyat. Tumepewa kalamu kama silaha ya kuwashinda wapinzani wetu. Leo kalamu hii imekuwa ya kimtandao kwa sura ya vyombo vya upashanaji habari kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano pamoja na mawasiliano ya satelaiti. Siku hizi pia maadui zetu wanatumia silaha hii hii ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutushambulia lakini hawatambui kwamba watafedheheshwa kwa njia ile ile kama kama ilivyokuwa katika zama za bwana wetu Mtukufu Hadhrat Muhammad (s.aw).

Hivyo, Khalifatul Masih V a.t.b.a anatualika tuungane bega kwa bege ili kutawanya nuru duniani kote, kiasi hiki kwamba giza litoweke.

Jukumu la kwanza ni kwamba tunatakiwa tutumie zana/ rasilimali/teknolojia hizi adhimu kueneza elimu, kufanya (tabligh), kujenga uelewa kuhusu ujumbe wa kweli wa Islam na kuhubiri mafundisho ya kweli ya Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Hili linaweza kufanyika kwa kuandika makala katika magazeti mbalimbali, majarida, blogs na mikutano.

Alhamdulillah, kizazi chetu kimeshakwenda hatua moja mbele. Tovuti kama YouTube ambayo haikuwa imeanzishwa na Seydna Ahmad (a.s), kwa sasa zimejaa picha za video zikitangaza kuhusu ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s). Kila muahmadiyya anajivunia kufungua mitandao hii na kukuta video za hotuba zilizotolewa na makhalifa wetu.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba huu ndio mwanzo tu, hatuwezi kuishia hapa. Jukumu letu ni kujitahidi kushiriki katika jihadi hii zaidi na zaidi, na kufanya uwepo wetu katika mtandao wa intaneti kuimarika zaidi. Tunatakiwa tuujaze mtandao kueneza mafundisho mema na tusiache mwanya kwa mashambulizi ya shetani.

Siku zote, Mamula wamejaribu kuidhuru Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya na daima wamekuwa wakishindwa. Wakati wa uhai wa Masihi Aliyeahidiwa (a.s) walifikiri kwamba sauti yake isingalivuka 'kuta' za Qadiani. Lakini angalieni jinsi Jumuiya hii ilivyoenea. Hizi ni Rehema za zama za kielektroniki/ TEHEMA, kwamba kupitia televisheni ya MTA, sauti ya Khalifatul Masih a.t.b.a imeenezwa kila pembe ya dunia na watu wapya wanaisikia na kuukubali ujumbe wake kila siku.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Bustani ya Washairi

SIARIDHII MAAZULI

1 Kwa jina lake Manani, Ambaye yu Akhiari
Alotukuka dayani, Asifiwa kila zuri
Msitawisha mbinguni, visiwa hadi barari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

2 Nawasalimu amani, ziwawie idhihari
Kwa salama salimini, mpwelewe tahayuri
Wasuna majumbani, kukicha msiuniri
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

3 Umaazuli wanini, hiyo kwangu si khabari
Kujipwekesha pembeni, silo jambo la umuri
Si hali ya muumini, imbali na Afkhari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

4 Ewe ghashi wa nyumbani, ulo kuwa na khiyari
Uwazaye mara thani, kijana alo nawili
Wa ukoo ahuweni, alosawa kitijari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

5 Kauli yapendwa nini, pesa indani suduri
Midirari mia thani, kitanda na mauthuri
Umui wautamani, takosa raha nuhuri
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

6 Muizzi ana thamani, jipatie ihrari
Uwe hasa mwanadini, uishi kwa tahadhari
Uwe ummi makini, kwa hilo sote tukiri
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

7 Kwa kijana mhisani, wa mawazo ya uturi
Ulo na wako kichwani, ati umemsetiri
Mlegevu wa uyuni, afananaje suari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

8 Moyoni wa msanii, yu malkia muniri
Mwenye rangi aluani, yu mrembo na abiri
Mh! yu hurul aini, usaili memkiri
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

9 Mawazo kuu kinzani, ati mpate sitari
Msabato kanisani, aje awe mhubiri?
Wajichinjia majini, tusi one ahmari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

10 Maisha ya ujanani, yameshitadi khatari
Umpate muumini, mpozwe na mistari
Sala ikimu ndani, yu aipenda jabbari
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

11 Mwisho nawaambieni, muitafute sitari
Muepushwe na tufani, za duniaze ghururi
Usitindanga zimani, baraka zijifiri
Siaridhii maazuli, ndoa nawahusiani

Mwl. Muhammad Habibu
Mlandizi – Pwani

NIISHI MAISHA GANI?

1 Haya ni maisha yangu, napaswa kuwaambia
Kumsifu Mola wangu, na makosa kutubia
Sipotezi siku yangu, kwa ujinga wa dunia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

2 Nimefunga ndoa yangu, na shekhe kahutubia
Hatutapiga uwangu, wala ngoma za bandia
Nimeachwa peke yangu, ndugu wamenikimbia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

3 Alfajiri ya Mungu, sote tumeamkia
Mimi na mke wangu, udhu tumejipatia
Uchawi ni sifa yangu, leo wamenipatia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

4 Nawapenda ndugu zangu, hasa Wanajumuiyya
Na hata jirani zangu, napita kusalimia
Lakini kuna mafungu, wengine waninunia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

5 Natoa michango yangu, kipato nikishatia
Namwita Katibu wangu, risiti kunikatia
Nikikumbusha wenzangu, wasema ninajitia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

6 Mikutano tawi langu, namimi nahudhuria
Ya utamu na uchungu, wote wana ichangia
Namimi nitoe yangu, watu wana nigunia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

7 Na majlisi yangu, twapanga twafurahia
Kila nyumba kwa mafungu, zote tunazipitia
Lakini kwa lulu wangu, maneno kanipakia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

8 Mahubiri nyuma yangu, wengine wanifatia
Natoa nasaha zangu, peperushi nazo pia
Na hata adui zangu, rehema nawatakia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

9 Si kinyume haya yangu, mitume wamepitia
Waliyapata machungu, majeraha kuwatia
Lakini waomba Mungu, misamaha kupatia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

10 Natii wakubwa wangu, lawama sijawatia
Ninawaombea Mungu, afya na muda pia
Kutimiza yake Mungu, maagizo ya masia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

11 Na hasa nafusi yangu, Nanyi wenzangu pia
Tuuwache ulimwengu, na madhila yake pia
Pamoja tufunge pingu, kwa Masihi wake pia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

12 Tuachane na mafungu, Mola Anayachukia
Wote tuwe na machungu, wapi tutapofikia
Moyo wauma wenzangu, hapa ninaishilia
Niishi maisha gani, Niipendeze dunia?

Haji H. Mbanga (Mvumilika)
Ikwiriri - Pwani

KHUDDAM TANGAMANENI

1. Tumshukuru rabuka, Muumba wetu jalali
Kwa wote mliofika, wa karibu na wa mbali
Kwa heshima natamka, karibuni tafadhali
Khuddam tangamaneni, Muikuze Jumuiya.

2. Leo ni siku adhimu, hapa tumekusanyika
Ninawaona khuddamu, wana furaha hakika
Basi si mtabasamu, takibira kutamka
Khuddam tangamaneni, Muikuze jumuiya.

3. Ni mengi mmejifunza, toka jana hadi leo
Na mimi nawahimiza, muyashike kama ngao
Msije kuyapuuza, mkose mafanikio
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

4. Kwa kuwa tumekutana, wacha tukumbushaneni
Tuwambizane ya maana, yakutujenga imani
Nasi tuwe waungwana, mbele ya Mola manani
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

5. Ninaanza na shahada, na sala simamisheni
Muifanye kuwa ada, na zaka pia toeni
Maana hatuna muda, tunapita duniani
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

6. Inapofika saumu, wakati wa Ramadhani
Fungeni huo msimu, na hija pia nendeni
Mana vyote ni muhimu, vya kuingiza peponi
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

7. Khuddam nawaimbia, nisikizeni vizuri
Kwenye hii Jumuiya, ni nyinyi wenye fahari
Mnategemewa pia, mje kuwa maamiri
Khuddam tangamaneni, muikuize Jumuiya.

8. Msione ninaimba, mwone nawafurahisha
Ujumbe wangu wajomba, nawapatia motisha
Ya kwamba mshike namba, mseme kuwa mwatosha
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

9. Sadar nisikilize, name nisome shajara
Naomba muyatimize, yalosemwa kwenye shura
Ili tuiendeleze, Jumuiya iwe bora
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

10. Wote waloshughulika, kwenye hii jitimaa
Mikakati wakaweka, na kisha wakaandaa
Nawaombea Baraka, Mola awape shufaa
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya

11. Kusimama nimechoka, nahisi kizunguzungu
Nawaomba kuondoka, mniruhusu wenzangu
Msije mkaboreka, mnitoe kwa marungu
Khuddam tangamaneni, muikuze Jumuiya.

Utunzi wa
Ismail M. Bakari (Swila mchiriza sumu)
Box 2108-00100 GPO
Nairobi-Kenya.

MOLA KAJIBU MAOMBI

1. Ze Holy Li-Quran, katuambia Manani
Nacho kipenda Rohoni, Kwa Mola ni mtihani
Nimesoma kwa makini, nisije kosa yakini
Ninahamia Mtwara Mola kajibu maombi

2. Maombi kwa Rahmani ,waweza ona matani
Jibu Iikiwa hewani, unashtuka moyoni
Nikagundua Manani, Anipeleka nyumbani
Ninahamia Mtwara Mola kajibu maombi

3. Nilijiona ndotoni, na mizigo mgongoni
Naelekea Kusini, naenda uhamishoni
Nikawaza kulikoni, nimekuwa hayawani
Nahamia Mtwara mola kajibu maombi

4. Fadhila za Ramadhani, na dua kwa Rahmani
Kanijibu faraghani, nikiwa usingizini
Inabidi niamini, niliyoona ndotoni
Ninahamia Mtwara Mola kajibu maombi

5. Ni siri toka moyoni, siwezi weka juani
Namshukuru manani, nifike zangu kusini
Siwezi jua mbeleni, mola katakia nini
Ninahamia Mtwara Mola kajibu maombi

6. Tabora nilitamani, na wala sio kusini
Nifike msikitini, pale Tabora mjini
Nikaibusu Quran, ilozikwa na wahuni
Ninahmia Mtwara Mola kajibu maombi

7. Siwezi leta kwa nini, kwa yale ya Rahmani
Sinung'uniki moyoni, vipi niende kusini
Alolipanga manani, ni bora sana mwishoni
Nahamia Mtwara Mola kajibu maombi

8. Mjumbe wa Kadian, kisha eleza zamani
Ombeni ndugu ombeni, maombi toka moyoni
Atawajibu Manani, mkiomba kwa yakini
-Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

9. Tatizo hapa mjini, ofisi zipo njiani
Tapangwa barabarani, asubuhi na jioni
Kienda msikitlni, unawekwa kitabuni
Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

10. Viongozi makazini, waangalia usoni
Wakiona huendani, na zao itikadini
Wanakuweka kundini, vurugu misikitini
Ninahamia Mtwara,Mola kajibu maombi

11. Siku zangu za mwishoni, kwa kazi barabarani
Umri nao mbioni, nijiandae shambani
Bora niende nyumbani, kuliko ughaibuni
Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

12. Kama sio Jamatini, ningaliweka ubani
Niwakumbuke majini, wanikinge safarini
Lakini kwa Jamatini, dua ni kitu makini
Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

13. Usia nawachieni, Kitonga nakwambieni
Tusifanyie matani, Kitonga si ugenini
Tukipaacha porini, Tuta chekwa ukubwani
Ninahamia Mtwara,Mola kajibu maombi

14. Ndugu zangu kwa herini, wa bara na visiwani
Taonana Jamatini, pia Kitonga shuleni
Inshalal iwe kinywani, tutaonana mbeleni
Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

15. Ndugu zangu karibuni, Polisi kule kusini
Kwa shida barabarani, Pigeni ya kiganjani
Sisi ni ndugu Jamani, sisite nipigieni
Ninahamia Mtwara, Mola kajibu maombi

16. Walahi mimi mgeni, kutokea kwenye fani
Nawaomba samahani, nilipoleta utani
Ni kama wa fomu wani, aanzapo darasani
Naenda zangu Mtwara, Mola kajibu maombi

SID C MASUD (AFANDE SAID)
POLISI TRAFFIC DAR ES SAALAM
(SAFARINI MTWARA)
0712-553196/0772-053196
0784-552104/0762-0691789

Maudhui na fani: *'Uongofu wa Tafsiri ya Qur'ani Tukufu*

Na Mahmood Hamsin Mubiru - Dar es salaam.

Kutoka Toleo lililopita

Tazama alivyochora taswira ya kitali toka mwanzo hadi mwisho, ingawaje kitali hicho ni cha kalamu. Uchaguzi wa msamiati unazidisha picha ya vita. Kwanza hili ni jeshi na jeshi hili ni Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Anayeliongoza ni Seyidna Ahmad (as) ambaye yeye ni Amiri Jeshi. Na mwandishi ni Askari katika kitali.

Msamiati mzima wa jeshi umetumika na msomaji toka mwanzoni kuwa jeshi hilo lililo katika mapambano ni mali ya mbora wa viumbe vyote Mtukufu Mtume Muhammad (saw). Hivyo msomaji anapewa bishara ya ushindi, kwani jeshi lenyewe ni la mtu mkubwa likiongozwa na mwanawe wa kiroho na askari ambaye yuko tayari kutoa maisha yake.

Shairi hili linampa hamasa msomaji kutaka kujua utakuwaje mwisho wa kitali -yaani mwisho wa vita.

Kwa kutumia rejea za wanazuoni waliobobea na wataalamu wa lugha, Sheikh Amri amethibitisha ya kwamba Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ni Mtume wa mwisho katika kuleta sheria na baraka hizo za utume zinapatikana kwa kumtii na kuwa mpenzi mkubwa wa Mtume aliyeitwa ni Rehema kwa walimwengu.

La kustaajabisha ni kwamba Sheikh Abdallah Saleh Farsy anadai ya kwamba Mtume Mtukufu Muhammad (saw) ni wa mwisho, lakini wakati huo huo anayo itikadi ya kuwa Nabii Isa (as) atarudi. Hapo Sheikh Amri anampa tahadhari na kusema;

Usemapo neno
pasi ujuzi mtimilifu,
Utauma meno
ujaposutwa udanganyifu,
Nayo matukano
mtukanayo na kukashifu,
Ndio msumeno
utakereza zenu sharafu.

Anamueleza kuwa haki ya kuandika au kuzungumza inapungua mtu anapokuwa hakufanya utafiti wa kutosha. Hayo hayo unayoyasema bila utafiti wa kutosha yatageuka msumeno wa kukereza zenu sharafu.

Ni shairi fupi lakini lenye ujumbe uliokamilika. Ni onyo ya kuwa haifai kujiingiza katika ngoma usiojua kuicheza. Kwani Waswahiil husema 'Mcheza hawi kiwete, ngoma yataka matao'. Lakumnusuru Sheikh Abdallah ni kumnusuru kuwa kiwete ki elimu na anaambiwa:

Elimu sikia
Zinahitaji kwingi kusoma,
Si za kuibia
Kijanja-janja na kunguruma,
Unachotambua
Ndiyo fikihi kuumauma,
Vipi kujitoma
Katika jambo usilojua?

Mambo ya ujanja ujanja, kubabia hayafai hata kidogo. Na mwisho wa ubeti anamuuliza swali ambalo anatakiwa alifanyie kazi. Vipi kujitoma katika jambo usilojua?

Kujitoma katika jambo usilojua ni dalili ya kuonesha ufupi wa elimu na ufupi wa elimu unafanya itikadi ya mtu iwe fupi. Sheikh Amri Abedi amesadifu jambo hili. Ubeti mtamu wa Seyidna Ahmad (as) unaosema;
Elimu ya mtu inapokuwa ndogo, itikadi yake pia itakuwa ndogo
Na kipofu hasifii uzuri, kwani ana udhuru wa kuwa haoni

Sababu zinazomfanya mtu huyu hatimaye awe kipofu ni kwa sababu ya uadui. Sheikh Amri amethibitisha ya kuwa masingizio aliyoyaleta Sheikh Abdallah kimsingi yanatokana na uadui alio nao dhidi ya Ahmadiyya. Hata ufanyeje uadui ukizidi basi huleta madhara makubwa na humuongezea husda na kumpeleka mbali. "Mtu huadui mwezi akauita ni nyota".

Kwa sababu ya uadui kazi yoyote uifanyayo adui hawezi kuona ni njema japo yeye kazi hiyo haiwezi. Ataipaka tope, ataichafua na ingawaje kila mtu anasisitiza kuwa 'huu ni mwezi' yeye atasema ni nyota. Ni shairi ambalo maneno yameteuliwa kwa umakini mkubwa sana na kwa jicho la fikra. Na tunamuona adui bila ya haya yoyote akiita mwezi nyota.

Sheikh Amri ameonyesha kuwa kazi ya kutetea Islam wamepewa Ahmadiyya. Hakuna anayeweza kuwanyang'anya baraka hii na heshima hii.

Methali. Methali ni maneno yenye hekima yaliyosheheni ujumbe mzito katika maneno machache. Methali zinatokana na uzoefu unaopatikana katika bahari ya maisha. Ni mtindo maarufu katika fasihi nyingi duniani. Mwandishi maarufu wa riwaya na mashairi katika Afrika Chunua Achebe anasema 'methali ni mafuta yanayolainisha maneno tayari kwa kuliwa'. Sheikh Amri amechagua methali ambazo zinasaidia kufikisha ujumbe uliokusudiwa lakini pia unampa furaha msomaji.

Katika utangulizi wa kitabu hicho ukurasa wa kumi na moja, Sheikh Abdallah Saleh Farsy anamuandikia barua Sheikh Amri na kumwambia kuwa amelazimika kuwapinga kwani 'ukimstahi mkendugu huzai naye'. Methali hii ni ujumbe kwamba hakuna njia yoyote nyingine ya kufanya isipokuwa kuwajibu ingawaje ninaelewa kuwa nyinyi ni masahibu wangu. Ni kweli Sheikh Abdallah Saleh Farsy aliwahi kumwandikia barua ya kupongeza kazi nzuri inayofanywa na Jumuiyya na hata katika utangulizi huo anamshukuru Sheikh Mubaraka Ahmad (HA) kwa kumpa nafasi "niandike kijitabu hiki cha kumjibu sahibu yangu Sheikh Abdallah Saleh Farsy wa Unguja." Inaonyesha urafiki wa Sheikh Amri na Sheikh Abdallah Saleh Farsy ni wa siku nyingi. Katika Diwani yake Sheikh Amri amenukuu mashairi ya Sheikh Abdallah Saleh Farsy kutoka kitabu chake 'Mawaidha ya dini' Bila shaka asingeweza kunukuu mashairi hayo bila ya ridhaa yake.

Kwenye ukurasa wa 37 Sheikh



Sheikh Kaluta Amri Abedi

Amri akieleza tatizo la kufunga milango yote ya rehema na elimu, Masheikh wamebaki katika maji mafupi kumbe kuna bahari kubwa ya elimu ambayo mvua bado inaendelea kunyesha kutoka mbinguni. Akina Sheikh Abdallah Saleh Farsy wanaendelea kuridhika na hicho kidogo walicho nacho, na ili kumfikishia ujumbe Sheikh Kaluta Amri Abedi anamfananisha na chura. "Chura aliyomo kisimani, hawezi kuelewa kiasi cha maji yaliyomo baharini". Ni hadithi ile ile ya kipofu alipata fursa ya kuona kwa sekunde mkonga wa tembo na macho yake yalipofumba kila alichoambiwa kwamba ni kikubwa aliuliza je ni kikubwa kama mkonga wa tembo?

Masihi Aliyeahdiwa (as) amekwishaleta bahari ya elimu. Unapoteza wakati wako ukiendelea kuoga kwenye bwawa. Methali hiyo inamtaka Sheikh Abdallah Saleh Farsy asiridhike na elimu aliyo nayo kwani elimu ni bahari katu hufiki pwani. Kama alivyoimba mwenye Sheikh Amri;
Toa waqfu ujana, elimu ukitamani,
Na uwe mzee sana, kujua usijihini
Elimu bahari pana, milele hufiki pwani.

Kwenye ukurasa wa 63 Sheikh Kaluta Amri Abedi amejenga hoja inayotokana na umahiri wa lugha, na anamtahadharisha kuwa ujanja ujanja hautafaa kitu, kwani neno 'Khatama' linapokuwa na 'Mudhwafu wa Mudhafu ilaihi' kwenye isimu za wingi kama lilivyo katika 'Khataman nnabiyyina' halijapa katika maandiko yote ya waarabu kuwa na maana ya mwisho. Hapo hapafai maneno bali kuvunja hoja. Neno la "Khatama" likifuatana na maneno ya wingi ambalo limepata maana ya mwisho. Sheikh Amri anasema katu hatafanikiwa na hivyo ubishi wake unakuwa wa kipuuzi na hapo ananukuu methali inayoonesha kujitia ujingani na kufanya jambo lisilo maana. "Pambani za mtonga maji ya dafu kuoshea donda".

Tashibiha. Tamadhali za semi ni maneno ambayo hutumiwa na muandishi ili kutia nguvu katika maana. Sanaa hii hutumika ili kupamba kazi ya fasihi, kuongeza mvuto au utamu wa lugha. Tashibiha ni moja ya tamathali za semi ambayo hulinganisha watu au vitu viwili na zaidi kwa kutumia maneno; "kama, mithili ya,...." Kwa ubingwa mkubwa sana Shehikh Amri ametumia tashbiha.

Katika utangulizi wa kitabu chake ukurasa wa 12 Sheikh Amri anamponda Muhsin Baruwani aliyeandika utangulizi wa kijitabu cha Sheikh Abdallah Saleh Farsy na kueleza kuwa Seyidna Ahmad (as) alizaliwa mwaka 1889. Sheikh Amri anampuuza kwani hata kama hajui Seyidna Ahmad (as) alizaliwa lini anawezaje kuandika chochote kinachohusu maisha yake? Hivyo akapuuza maneno yake; "Kama ya mtu asiye na akili ambaye amekokotwa tu ndani ya ngoma asiyojua kuicheza". Umewahi kuona mtu ambaye anajitoma katika jambo asilolijua? Anakuwa kichekesho kiasi gani mtu kuingia katika ngoma asiyojua kuicheza. Na hiyo ndiyo taswira tunayopata kuhusu ndugu Ali Muhsin Baruwani. Akifafanua juu ya waliyoisifu tafsiri ya Ahmadiyya na kuipa sifa tele, Sheikh Amri anasema walifanya hivyo kwani; "Wao ni mafasaha wa maneno, na maneno yetu hunyooka kama miali ya nuru". Hunyooka hivyo kwa sababu kila neno wanalolitoa linakuwa na ushahidi ulio wazi ambao unawafanya wenye kijicho waendelee kuumia.

Sheikh Amri anasema, Sheikh Farsy ameleta mashtaka mengi juu ya aya ya 7 ya sura ya 61, As - saf. Sheikh Amri hana mengi ya kusema isipokuwa msifuate maneno ya mtu huyu kama kipofu. Angalau kipofu ana udhuru.

Nia ya Sheikh Farsy siyo kutafuta haki na ukweli bali, kujifaharisha na husda ndivyo vinavyomtuma kupiga kelele za kijahili kama mtu aliyeshtuka kutoka usingizini. Katika vitabu hivyo 12 hakuna hata kimoja alichokigusa bali amebaki kupiga kelele kwamba naye anavyo. Majibu yake yanaonesha kwamba hayasoma vitabu hivyo 12 ila kelele zake ni za aliyeshtuka kutoka usingizini.

Dalili zote zinaonesha kuwa Sheikh Abdallah Saleh Farsy anakubali kuwa Ahmadiyya inatetemesha Ukristo ambao unashambulia dini ya Islam. Na hii inatokana na ujuzi wa Qur'an Tukufu na ujuzi ambao Jumujuiyya inao. Sheikh Amri anasema je Shekh Farsy anawezaje kudiriki kuparamia Ahmadiyya yenye nguvu namna hiyo. Anamlinganisha na ujinga wa chungu kupamia jiwe. Lakini kupamia kwake ni kama wasemavyo waswahili "Mpiga ngumi ukuta huumiza mkonowe".

Mambo kama huyawezi usijitome kama alivyosema Muyaka;

Msiyatwae kwa pupa, fikirini mkiwaza
Mkane yenu mishipa, katika wamba wa kiza
Yasije yakawakuta, mambo yakawaangamiza

Sheikh Amri anaonesha ya kwamba uwezo wa kufikiri wa Sheikh Farsy ni mdogo sana. Hawezi kuchambua mambo. Hawezi kutoa mawazo yake. Hayuko tayari kutofautiana na wengine wakati hiyo ni rehema, kama alivyosema Mtukufu Mtume Muhammad (saw); "Kutofautiana kwa Maulamaa wangu ni rehema". Islamu inaruhusu kujenga hoja. Inaruhusu kutofautiana katika rai. Sheikh Farsy haelezi maoni yake wala fikra, kila anapoulizwa anasema fulani alisema hivi, je yeye anasemaje? Kwa sababu ya mwenendo huu Sheikh Amri anamfananisha Sheikh Farsy na santuri ambayo inatoa kile kilichoko kwenye santuri ile bila fikra zozote. Ingelikuwa siku hizi Sheikh Amri angelisema kuwa Sheikh Farsy ni roboti.

Kilele cha ujuha wa Sheikh Farsy unabainishwa na Sheikh Amri anapotoa picha ya Shehikh Farsy ya kusikitisha. Yeye anaamini kuwa Mtume Muhammad (saw) ni wa mwisho, na wala hatakuja Mtume mwingine na wakati huo huo anaamini kuwa Nabii Isa (as) atarudi. Upotofu ulioje! Ujinga ulioje! Na ndiyo maana akamfananisha na mtu aliyekaa mtini juu huku anaukata shinani. Bila shaka kinachomsubiri Bwana huyu ni kuanguka na kupata mweleka wa kutia haya.

Tashtiti. Niuliizaji wa swali ambalo tayari lina jibu. Hivyo tashtiti hutumika ili kuweka mkazo wa jambo. Kukumbusha na kukebehi. Ni njia inayotukumbusha ili tusighafirike. Kwa ufundi mkubwa Tashtiti imetumika vilivyo katika Uongofu wa tafsiri ya Qur'an Tukufu.

Sheikh Kaluta Amri Abedi mwanzoni mwa kitabu chake anatoa ushahidi wa Waislam wataalamu na maarufu ambao wametoa ushahidi wa utume kuendelea na kwamba utume uliokatika ni ule wa kuleta sheria. Anawataja Waislam maarufu kama Muhyuddin ibn Arab, Sheikh Jeilani, Imamu Shaarani hao ni Waislam mashuhuri na wanaoheshimika kwa maskhara na kebehi anamuuliza Sheikh mkuu wa Unguja "Je hawa si Waislamu?" Kwa kutumia Tashtiti anamuuliza Sheikh Farsy je Sheikh Abdulqadri Jeilani je hakuwa Muislam? Je Sheikh Muhyuddin aliyeandika maneno haya hakuwa Muislam? Je Sheikh Imamu Shaarani naye hakuwa Muislam kwa kuandika kuwa utume uliokatika ni wa sheria tu. Sheikh Abdallah Saleh Farsy atawatoa Mawalii hawa na Maimamu hawa katika Uislamu? Je yeye anajua hata nusu ya elimu yao? Kwa sababu ya kusema neno pasi ujuzi mtimilifu, Shehikh Abdallah ameandika kuwa kila kitabu toka mwanzo mpaka leo kinasema kwamba hakuna atakayepewa utume tena. Tatizo la kusema bila kufikiri. Na hapo Sheikh Amri alipata fursa nzuri ya kumtupia mshale wa Tashtiti. Je ni kweli kuwa kila kitabu kilichoandikwa na Waislam kililazimika kueleza hiyo itikadi yake? Kebehi na kijembe cha kukata na shoka.

Uandishi ni sanaa, unalazimika kuwaelimisha watu na unalazimika pia kuwapa burudiko. Katu hayapendezi malaji yasiyo na badiliko. Shurti wali wa maji na wa pilau uwepo. Sifa hizi kwa kiwango kikubwa amezichuma Sheikh Kaluta Amri Abedi katika utungo wake "Uongofu wa Tafsiri ya Qur'an Tukufu na husda ya Sheikh Abdallah Saleh Farsy".

"Mwelewe Maulvi Nuruddin"

Hadhrat Khalifatul Masih I r.a.

Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. na kutafsiriwa kwa Kiswahili na Sheikh Jamil Rahman Rafiq

Kutoka toleo lililopita

MAWAIDHA YA MWISHO/ KUMBUKUMBU YANGU

Baada ya Mkutano akaandika kumbukumbu ifuatayo:

"Mungu Mtukufu Amesema katika Qur'an Tukufu: kama mkishukuru kwa neema zangu, Nitawazidishieni (14:8). ShuQur'an kwa neema za Mungu zinakuwa chanzo cha neema nyingine zaidi. Kwa hiyo, kwa kuthamini fadhili za Mungu naeleza shuQur'an yangu kwa Mungu kwamba Yeye ndiye Mkarimu kwetu sisi.

Mnamno mwaka huu baadhi ya wajinga walijaribu kuleta msukosuko katika Jumuiya, na kwa shabaha hiyo wakaeneza vijitabu vilivyoitwa *Idh-harul Haq,* ambamo mimi pia nikafanywa lengo la lawama. Shabaha ya mtungaji wa vijitabu hivyo ilikuwa kueneza mfarakano katika Jumuiya. Lakini Mungu kwa fadhili yake Akailinda Jumuiya na mimi pia katika fitina yake. Msaada Wake na nusura Yake ikadhihirishwa kwa namna ambavyo mipango yote ya wafitini ikavunjika kabisa na Jumuiya ikakingwa isipate madhara. Hiyo ikathibitishwa hadharani katika siku za Mkutano wa Mwaka. Hili lilikuwa dhihirisho maalum la msaada na nusura ya Mungu Mweza ya kwamba ijapokuwa zilikuwapo sababu kadha zenye kisirani na uenezaji wa vijitabu vyenye kusumbua vilivyoitwa *Idh-harul Haq,* mahudhurio katika Mkutano yalikuwa makubwa zaidi kuliko miaka iliyopita. Nyuso za washiriki zilidhihirisha mapenzi na uaminifu ulioshuhudia bayana kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya inakingwa kikamilifu dhidi ya kila athari mbaya. Aidha, matawi mbalimbali ya Jumuiya yaliweka mfano mwema wa kujitolea ambao ndio ushuhuda wa fadhili ya Mungu isiyo na kifani. Mnamo mwaka huu Jumuiya ilitimiza wajibu mzito wa kutoa michango, hata hivyo *Sadr Anjuman* ilikuwa na hasara. Matawi yalichukua, kwa uchangamfu na furaha, jukumu la kuondoa hasara, na fedha nyingi taslimu zilichangwa. Kwa jumla fedha zilizoahidiwa na kutolewa zilikuwa mara tatu kuliko zilizochangwa mwaka jana, jambo linaloonekana ni fadhili kubwa za Mungu, tukiona kwamba idadi ya wanajumuiya ni kidogo tu.

Mkutano pia ulikanusha vizuri sana masingizio ya wale walioeleza kwamba kuanguka kwangu kutoka juu ya farasi jike kunamaanisha kuondolewa kwangu katika cheo na heshima ya kuwa *Khalifa*. Msukosuko ulipoanza dhidi ya *Ukhalifa*, Mungu Akanionyesha katika ruya kwamba nikiwa juu ya farasi napitia nchi iliyo kavu na kame. Nikamwendesha farasi mbele naye akaanza kukimbia mbio sana hata ikawa vigumu kwangu kumuweza, lakini kwa fadhili ya Mungu nikaendelea kukaa juu yake kwa imara. Baada ya mwendo mrefu, farasi akaingia katika bonde lenye rutuba ambako kila mahali ilionekana migunda futi mbili juu. Farasi akaendelea kukimbia mbio, na alipofika katikati ya bonde nikazinduka. Kutokana na ruya hiyo nikafahamu kwamba wale wanaodai nitaondolewa katika cheo cha *Ukhalifa* watathibitika kuwa waongo, na kwamba si tu Mungu Atanitetea, bali Atanijaalia ufaulu. Ni fadhili ya Mungu kwamba Ametimiza ruya yangu hii pia. Mkutano wa Mwaka, wa mwaka huu, umehakikisha kwamba ruya hiyo ilikuwa ya kweli. Juu ya upinzani na uenezi wa vijitabu bila jina la mtungaji, Amedhihirisha msaada baada ya msaada, Ameongeza mapenzi na uaminifu nyonyoni mwa wanajumuiya, Amevuta nyoyo zao kwangu, kawatilia roho ya utii mioyoni mwao na Amewakinga dhidi ya hila za wafitini"

Mnamo Februari 2, 1914, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alitoa agizo:

"Kumbukeni, watoto wangu wasipewe chochote katika mali ya sadaka au zaka, au katika mali yoyote iliyowekwa kwa ustawi wa mayatima au maskini. Mungu Atawajaalia riziki. Yeyote atakayeandika habari za maisha yangu apaswa kutaja agizo langu hili na ajizuie kulivunja. Sina fedha. Madeni yangu yote yamelipwa. Sidaiwi na yeyote. Mtu yeyote asiwadai chochote watoto wangu."

XVII
KUMBUKUMBU YANGU

Baba yangu Chaudhri Nasrullah Khan, alikuwa mwanasheria (wakili) aliyekuwa anafanya kazi katika Sialkot, Panjab. Mwanzoni mwa karne hii, yeye aliajiriwa kutetea daawa ambamo maswali ya kuvutia na kukanganya yalizuka yaliyotakiwa kuamuliwa na mahakama. Miaka kadha hapo kabla, Maulawii Mubarak Ali, Imam na Msimamizi wa Jamia Masjid wa Sialkot Contonment, alijiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya; msikiti huo ulikuwa mkubwa sana na uliwekewa wakfu mali nyingi. Itikadi zake zilizolaumiwa vikali na Masheikh wa kisuni, zikawa chanzo cha uchungu na mahangaiko kwa wale waliokuwa wanasali humo msikitini, ambazo pole pole zikawa sababu ya kutokuvumilia na uadui. Hatimaye watu kadha miongoni mwao wakapeleka mashtaka mahakamani kutaka kwamba itangazwe ya kuwa kwa sababu ya kujiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya mshtakiwa, Maulawii Mubarak Ali, ametoka katika Islam, kwa



Maulana Hadhrat Hakeem Nuruddin Khalifatul Masih I r.a.

hiyo hafai kufanya kazi kama Imam au Msimamizi wa Jamia Masjid. Kulikuwa hakuna wakili Ahmadiyya mjini Sialkot katika zama hizo; baba yangu akaajiriwa kuwa wakili wa mshtakiwa. Yeye akataali kwa makini sana na kwa ukamilifu maswali ya kidini yaliyoulizwa na wenye kushtaki kuimarisha madai yao ya kwamba Ahmadiyya hawezi kufikiriwa kuwa Mwislamu; akawa na moyo wa huruma kwa maoni ya Waahmadiyya. Jambo jingine lililomwathiri sana lilikuwa kwamba wadai na mashahidi wao wakitoa ushuhuda kwa kuapa hawakusita kusema uwongo au kugeuza habari kama wakiona majibu yaliyo sawa yaweza kudhuru kesi yao; lakini mshtakiwa na mashahidi Waahmadiyya wakashikamana na ukweli bila kujali maneno yao yataiathiri vipi kesi yao. Akafikiria kwamba kiwango cha juu cha khulka njema za Waahmadiyya zilizodhihirika kwa namna ya kustaajabisha ni dalili kwamba msingi wao ni katika ukweli. Uchunguzi wa hakimu ukathibitisha mshtakiwa ndiye mwenye haki, kwa hiyo kesi ikafutwa. Wadai wakakata rufaa dhidi ya hukumu ya hakimu, lakini rufaa nayo ikafutwa. Jambo hilo likamwelekeza baba yangu kwenye Ahmadiyya.

Baada ya muda kidogo akaitwa kuhudhuria kama shahidi wa mshtakiwa katika Kortiya Hakimu mjini Gurdaspur katika kesi ya jinai ambamo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya, alishtakiwa kumwumbua Maulawii Karam Din, adui mmojawapo mkali mno. Hiyo ikampatia nafasi ya kuonana na mtu mtukufu, naye akaathirika sana na utakatifu wake.

Katika kipindi hicho, mnamo kiangazi cha 1904, mama yangu asiyekuwa na uhusiano na Ahmadiyya wala hakuwa na habari ya Jumuiya hiyo, ingawa muda kidogo hapo kabla baba yake na ndugu yake wa pekee walijiunga katika Ahmadiyya, akajaaliwa kuona ruya zenye maana sana za kiroho ambamo aliwahi kumwona mtu mmoja mkubwa mtukufu ambaye, mama alifikiri, alitaka kumwongoza katika njia ya wema. Ruya hizo zikamchangamsha na kumwathiri mno moyoni. Hakujua asilani yule mtukufu alikuwa nani, na katika ruya ya tatu akamwomba amweleze yu nani. Akamwambia, yu Ahmad. Alipomweleza baba yangu, yeye akasema kwamba kwa kuwa Ahmad ni jina moja la Mtume Mtukufu s.a.w. wa Islam, pengine mama amebahatika sana kujaaliwa kumwona yeye kiroho. Lakini mama akamweleza kwamba yeye anahisi kwamba mtukufu ambaye yeye alimwona katika ruya zake anaishi katika zama hizi ambaye anaongozwa naye katika ukweli na wema. Baada ya siku chache nduguye akaja kumtembelea na aliposikia ruya yake ya mwisho akasema Ahmad ni jina la Masihi Aliyeahidiwa na kwamba wewe umemwona yeye tu ndani ya ruya zako. Mama akasema ana yakini kwamba Mungu Aliyechagua njia hii ya kumwongoza, Atamweleza katika muda ufaao shabaha Yake kwa uwazi zaidi.

Ilitangazwa ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. yuko Lahore matembezini na kwamba hotuba yake itasomwa huko Lahore tarehe 3 Septemba 1904, naye atakuwapo hapo mwenyewe. Baba yangu akaenda Lahore kwa shabaha hiyo, na kwa bahati njema sana akanichukua pia pamoja naye. Pindi nilipotazama uso uliobarikiwa wa mtukufu huyo, nikafurahishwa mno, na muda wote alioendelea Maulawii Abdul Karim kusoma hotuba, nikaangazia macho uso wake ung'aao. Ukweli wake ukapenya moyo wangu na roho yangu nami nikahisi kwamba nimejitolea kwake kabisa. Nilikuwa mwanafunzi tu wa shule, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, lakini nilikuwa na yakini kwamba Mungu Amenibariki sana mno kwa fadhili zake kwa kunijaalia nafasi hiyo njema.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawasili Sialkot matembezini tarehe 27 Oktoba 1904, pamoja na watu wa familia yake na baadhi ya wafuasi wake akiwemo Maulawii Nuruddin r.a. Keshoye asubuhi, baba yangu alipokuwa akijitayarisha kwenda kortini, mama yangu akamwuliza, je, naweza kwenda kumtazama mgeni mheshimiwa na kumwona kama ni yule yule mtukufu nimwonaye katika ruya.

"Nenda kwa vyovyote," akasema, "Ukachunguze, lakini usifanye uamuzi wa mwisho."

"Kama ndiye huyo huyo, nitakosea machoni mwa Mungu, nikibaki nyuma baada ya mwongozo wa wazi Alionijaalia."

"Hili ni jambo la muhimu sana, nami sipendi tufarakane juu ya hilo. Ujuavyo, ninaendelea kuisoma habari hii. Tutazungumzia habari hii pamoja, na ninafikiri tutafikia uamuzi huo huo."

"Wewe umesoma sana, nami sikuwahi kusoma vitabu. Lakini nafikiri Mungu kwa fadhili Yake Amechagua njia Yake kuniongoza. Nikiona mwongozo Wake unaashiria upande huu, lazima nisogelee ipasavyo. Kama ni vingine, nitafurahi kuzungumza habari hii nawe na twaweza kuamua pamoja."

"Kukawia kidogo hakudhuru. Nahofia kufarakana juu ya swali hili la muhimu kabisa."

"Nimekwisha kuambia nifikirivyo."

Nikafuatana na mama yangu alipoondoka kutafuta alichothamini sana ambacho alisukumwa kwacho na roho yake. Alipofika nyumbani alimokaa Masihi Aliyeahidiwa a.s. pamwe na ahali zake akahudhuria mbele ya Hadhrat Ummul Muminin na kumwomba amfanyie mpango ili aweze kumtazama mara moja mumewe mtukufu. Akapelekewa ombi, naye akarudisha jibu kwamba baada ya muda kidogo atapitia hapo na atakawia kwa dakika chache akielekea msikiti wa jirani ili kushiriki kusali. Halafu akawasili na kuketi karibu na Hadhrat Ummul Muminin, futi chache kutoka alipokaa mama yangu pamoja nami. Alipomwona tu, uso wake ukang'ara na kwa tabasamu yenye jazba akasema: Bwana wangu, ningependa kufanya baiati. Akakubali kwa ukarimu: "Kariri nyuma yangu nitakayosema." Kisha akatamka fungu kwa fungu maneno ya ahadi ya baiati na mama akakariri nyuma yake. Mwishowe akafanya maombi ya kimya ambamo ahali zake, mama yangu na mimi tukaungana naye, na yeye akaondoka. Nikapata kujua baadaye kwa sababu ya kuchunguza mwenyewe kwamba hiyo ilikuwa si kawaida ya Masihi Aliyeahidiwa, hususan aliyekuja kufanya baiati akiwa mwanamke ambaye mumewe hakuwa mwanajumuiya wa Kiahmadiyya, Swali lolote halikuulizwa na pande zote mbili, halikutamkwa hata neno moja zaidi ya maneno maalumu ya ahadi ya baiati. Ilionekana kuna mwafaka mtimilifu baina ya atafutaye na atafutwaye. Roho ya mama yangu ikapata utulivu, utafiti wake ukamwongoza kwenye pepo zake za kiroho. Hakumwona tena isipokuwa katika ruya, lakini kujitolea kwake kulidumu kikamilifu na kwa uhalisi katika majaribio na mateso yote mpaka pumzi yake ya mwisho aliyopumua katika hali ya kufahamu, zaidi ya theluthi ya karne baadaye.

Itaendelea toleo lijalo, Inshallah

Safari ya Sadr Khuddam katika mikoa ya kanda ya kati na kanda ya magharibi

Na Mwandishi wetu -
Dar es salaam

Kutoka Toleo lililopita

Sadr Khuddam akieleza machache kabla ya kuwasilisha ujumbe maalum aliokwenda nao, alisema kukanyaga ardhi ya Tabora na bilkhusus katika Msikiti ule kumemkumbusha mbali takriban miaka 25 iliyopita wakati huo akiwa Atfal na baadaye Khuddam katika tawi hilo. Sadr alisema mengi ambayo amekuwa akiyafanya hasa kitanzim alifundishwa katika tawi hilo kipindi ambacho Sheikh Yusuf Athumani Kambaulaya na baadae Sheikh Fayaz wakiwa ni wabashiri. Alikumbusha shughuli za Mahubiri, Waqar Amal na Darasa la Qur'an Tukufu enzi za wakati wao, aliwataka Khuddam wasimame imara kuhakikisha shughuli za Tanzim na za Jamaat zinasonga mbele badala ya kumuachia Mwalimu pekee aendeshe shughuli hizo. Hivyo Khuddam wajue wanao wajibu mkubwa kutekeleza shughuli hizo kwani wao ndio uti wa mgongo wa Jamaat. Na katika kutekeleza mipango ya kitanzim ni wajibu wa Khuddam kuhakikisha Atfal wanashirikishwa ili kuwajenga na kuwapa uzoefu. Muhtamim Atfal alikazia.
Kikao kilifungwa kwa maombi baada maoni na shukrani zilizotolewa na Ansarullah, Mzee Bundala na Bw. Yunus.

Tarehe 22/05/2012 msafara wa Sadr uliondoka Tabora mjini saa mbili asubuhi kuelekea Jamaat ya Ulyankulu. Alhamdulillah, msafara ulifika salama, na kulakiwa na Mwalimu wa kujitegemea Mwl. Mussa Saidi pamoja na Khuddam. Ulyankulu ina matawi mawili - Ulyankulu Kaswa na Ulyankulu Mbeta. Matawi yote haya yanasimamiwa au kongozwa na Mwalimu wa kujitegemea ambaye pia ni Rais wa Tawi la Kaswa - Mwalimu Mussa Saidi. Pamoja na yote kimkoa Ulyankulu ipo chini ya Mbashiri wa Mkoa wa Tabora Mwalimu Othumani Yusuf Mawingu. Kikao kiliendeshwa sawa na utaratibu, na baada ya kikao, chakula pamoja na sala, Sadr na ujumbe wake walioneshwa kiwanja pamoja na matofali ya kuchoma yaliyoandaliwa kwa ajili ya ujenzi wa Msikiti. Kiwanja kipo eneo zuri pembeni ya barabara kuu inayotoka Tabora mjini kuingia Ulyankulu. Majira ya saa tisa Sadr na ujumbe wake waliagana na wenyeji na kuanza safari ya kuelekea Urambo.

Jamaat ya Urambo inaongozwa na Mwalimu Bakari Ally ikiwa na jumla ya matawi matano. Matawi hayo ni Urambo mjini, Mpigwa, Igwisi, Itundu na Kasisi. Kikao kilifanyika katika tawi la Itundu kwa kuyashirikisha matawi yaliyobaki. Pamoja na utekelezaji wa shughuli za Jumuiyya pia matawi haya yanakabiliwa na changamoto nyingi. Baadhi ya mambo Sadr sahib aliyatolea ufafanuzi na mengine ni ya utekelezaji kiofisi Sadr aliahidi kuyashughulikia.

Tarehe 23/05/2012 msafara uliondoka Urambo saa mbili asubuhi kuelekea Nguruka. Baada ya saa mbili na nusu kupita vijiji, miji na pori kubwa la Usinge, njia panda ya kwenda Kigoma na kuingia Nguruka mjini, msafara wa Sadr ulisimamishwa na kundi la watu. Watu hao hawakuwa wengine bali ni Wanajumuiyya wa tawi la Nguruka. Khuddam kwa Ansarullah bila kuwasahau Atfal -ul- Ahmadiyya, wakiwa wamevalia mavazi nadhifu, walijipanga mstari huku wakinyanyua mikono na kutoa heshima ya Ahlan wasahlan wamarhaba. Walisalimiana na ujumbe wote kwa mapenzi makubwa na baada ya hapo uongozi pamoja na Wanajamaat wote walimuongoza Sadr na ujumbe wake kuelekea tawini kwa miguu huku wakipita katikati ya viunga vya mji wa Nguruka kwa umbali wa kilomita mbili (2). Hakika heshima, mapenzi na thamani juu ya uongozi ilidhihirishwa na Wanajumuiyya hawa kwa kiwango cha hali ya juu bila kujali heshima na madaraka waliyokuwa nayo baadhi yao katika mji wao.

Baada ya sala ya Adhuhuri na Alasiri, Sadr na ujumbe wake walitembelea familia baadhi za Wanajumuiyya na familia ya mwisho ilikuwa ya Bw. Khamisi Mohamedi Msimbe ambapo matayarisho ya chakula cha mchana yaliandaliwa hapo. Jamaat ya Nguruka inao msikiti mzuri unaopendeza kwa muonekano wake. Jamaat hii ina matawi mawili. Tawi la Nguruka na tawi la Lugongoni na yote yapo chini ya Mwalimu Iddi Nuhu Sango. Kikao kilifanyika Msikitini saa tisa Alasiri.

Katika risala ya Qaid wa tawi Bw. Rubanga Jafar, alieleza utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Jamaat zinazofanywa na Khuddam katika tawi lao. Kama Waqar Amal iliyofanywa katika kituo cha Polisi cha Nguruka, Khidmat Khalq (huduma kwa viumbe) katika kituo cha afya na kwa mahabusu katika magereza ya hapo. Pamoja na hayo, ibada ya sala, utoaji wa michango na mahubiri vinatekelezwa ipasavyo.

Hakika risala ilionesha uhai mkubwa uliokuwepo katika Tanzim ya Khuddam hapo tawini. Na hii yote ni uthibitisho wa uongozi bora na imara wa Rais wa Mkoa ambaye anaishi hapo Mzee Moshi Mohamed Msimbe. Baada ya Sadr kuwasilisha aliyowapelekea kikao kilifungwa na safari ya kwenda kuangalia eneo la Jamaat lenye heka 3 ilianza. Eneo lipo sehemu nzuri pembeni ya barabara kuu ya kwenda Kigoma Mjini.

Tarehe 24/05/2012 kabla Sadr na ujumbe wake hawajaondoka Nguruka, kulikuwa na ratiba ya kutembelea Ofisi za Serikali hapo Nguruka. Kwanza Sadr alitembelea kituo cha afya. Baada ya kuongea mawili matatu, na Mganga Mkuu pamoja na kusaini kitabu cha wageni, Sadr na ujumbe wake walitembezwa idara chache kituoni hapo. zilifuatia Ofisi za Serikali ya Kijiji. Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji ni Ahmadiyya Bw. Yaqub Mussa Nzigamiye. Hapo Sadr alitambulishwa kwa Bwana afya na mtendaji wa hapo. Baada ya kusaini kitabu cha wageni, msafara uliekea kituo kikuu cha polisi Nguruka. Ujumbe mzima pamoja na wenyeji ulikaribishwa Ofisini kwa Mkuu wa Kituo ambae alishukuru kwa kutembelewa na watu wa dini tena kutoka Makao Makuu. Baada ya maongezi machache Mkuu huyo hakuruhusu ugeni huo uondoke bila takrima. Ama kwa hakika ilikuwa ni mshangao wa mwaka. Sehemu ambayo hufahamika kuwa ustarabu na ubinadamu ni adimu kupatikana, wajumbe wa Masihi (a.s) walifanyiwa takrima. Alhamdulillah. Hatimae msafara ulielekea Uvinza sehemu maarufu katika Mkoa wa Kigoma kwa utengenezaji wa chumvi.

Mandhari ya mji huu ni mabonde na milima. Sehemu ambayo Wanajumuiyya huendesha shughuli za Jamaat ni katika kilima kilicho pembezoni kidogo mwa barabara kuu iendayo Kigoma. Jamaat haina Msikiti hapo, hivyo shughuli zote za Jumuiyya hufanyika nyumbani kwa Rais wa tawi hilo. Hata hivyo wanacho kiwanja pamoja na mawe ya kutosha na wanataraji kuanza ufyatuaji wa matofali kwa ajili ya ujenzi huo.

Msafara wa Sadr ulipokewa na Wanajumuiyya wote kwa ujumla. Ansarullah, Khuddam na Atfal walikutwa katika barabara kuu pindi msafara wa Sadr ulipowasili. Sawa na Jamaat zilizotangulia, kikao kiliendeshwa kwa kufuata taratibu zote. Baada ya kikao Sala pamoja na chakula vilifuatiwa na hatimae msafara uliondoka kuelekea Kigoma.

Tarehe 25/05/2012 mara baada ya sala ya Ijumaa kikao cha Tanzim kilianza rasmi. Khuddam 18 na Atfal 9 wakiongozwa na Mwalimu Musa Kaswezi ambaye ni Mbashiri wa Mkoa wa Kigoma walihudhuria. Akiwasilisha risala kwa niaba ya Qaid wa tawi Mwl. Mussa Maswezi alisema, kipindi amehamia hapo kuwa Mwalimu wa tawi walikuwa Khuddam watano (5) kutokana na mahubiri aliyoyasimamia hususan nje ya mji ndio yameleta matunda yanayoonekana sasa. Mwalimu alisema ameanzisha darasa la masomo ya dini katika kijiji cha Lubengela hata hivyo zipo changamoto chache zinazomkabili kama vile ukosefu wa vitabu na dawati za kukalia. Sadr akijibu risala yake alimwahidi kushirikiana naye ili kuhakikisha kuwa changamoto hizo zinaondoka. Tarehe 25 na 26 haikuwa na kikao chochote, bali Sadr alitumia muda huo kusalimia ndugu na jamaa ikizingatiwa kuwa Kigoma ndipo asili yake, mahali alipozaliwa na kupitisha maisha machache ya mwanzoni ya utotoni mwake.
Tarehe 27/05/2012 msafara uliondoka Kigoma kupitia Nguruka, Tabora na hatimae tarehe 29 uliwasili Kinyento Kilometa chache kutoka Singida mjini. Mwalimu wa tawi Ramadhani Mrisho aliwaongoza Wanajumuiyya kuupokea msafara wa Sadr Khuddam. Kikao kiliendeshwa sawa na taratibu. Baada ya chakula, Sadr na ujumbe wake waliombwa kwenda kuwasalimia wanakwaya ya chama cha Mapinduzi ambao walikuwa wanafanya matayarisho kwa ajili ya kusherehekea ushindi wa Mwenyekiti wa serikali ya kijiji kutoka chama chao ambaye pia ni Ahmadiyya. Sadr alipata sunna aliyoipata Mtukufu Mtume Muhammad (saw) ya kupokewa kwa vigoma. Baada ya utambulisho kwa pande zote na Sadr kusema maneno machache, ruhusa ilitolewa na safari ya kuelekea Manyoni ilianza majira ya Magharibi.

Msafara uliwasili Manyoni majira ya saa mbili za usiku. Mara baada ya sala kikao kilianza. Tawi la Manyoni bado ni tawi changa likiwa chini ya Mwalimu Khalifa Jailani. Tawi lina Khuddam 4 na Atfal 3. Kikao kilifuata utaratibu mzima sawa na vikao alivyoendesha Sadr katika matawi mengine. Kikao kilifungwa kwa maombi, yaliyo ongozwa na Sadr.

Kikao cha mwisho kilifanyika Dodoma Mjini tarehe 30/05/2012 saa nne asubuhi mara tu baada ya kuwasili kutoka Manyoni. Naib Qaid Bw. Abdallah Mgunya akiwaongoza Khuddam wa tawi hilo walisikiliza kwa makini mipango yote iliyowasilishwa na Sadr. Akisisitiza suala la mahubiri, katibu wa Tabligh Bw. Salum Ibrahim Ndatama alisema; Ni wajibu kwa Khuddam kufanya mikakati madhubuti ya kufanya mahubiri katika maeneo yao. Mahubiri yatawapa mshikamano, yatawaongezea elimu yao ya dini na pia watakuwa wametimiza agizo la Mwenyezi Mungu la kuita watu katika njia yake. Na pindi watakapopanga mipango yoyote na wakaona inahitajika nguvu ya wahubiri kutoka Makao Makuu wasisite kusema. Na jambo zuri ni kutuma taarifa za mahubiri yote Makao Makuu. Mwisho kikao kilifungwa kwa maombi majira ya saa sita mchana.

Sadr Khuddam na ujumbe wake walifanya vikao 10 vilivyojumuisha matawi ishirini na tatu (23) na jumla ya Khuddam na Atfal waliokutana nao ni 150. Msafara ulirejea Dar es salaam jioni ya tarehe 30/05/2012. Alhamdulillah.

Akielezea muhtasari wa ziara yake, Sadr Khuddam alisema, kwanza shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwawezesha kutimiza nia yao kwa kwenda salama na kurudi salama. Pili alitoa shukrani kwa Masheikh, Waalimu, Marais na Maqaid wa Khuddamul Ahmadiyya katika matawi aliyotembelea kwa ushirikiano waliompa hata kufanikisha ziara na vikao vilivyofanyika katika matawi yao.

Sadr alitoa shukurani kwa Khuddam na Atfal wote pamoja na Ansarullah ambao hawakuwaacha wana wao katika vikao vyao. Na shukrani za dhati Sadr alizitoa kwa Lajna Imaillah kwa mchango mkubwa (wa utayarishaji chakula) waliotoa katika kufanikisha ziara hiyo.

Sadr alisema kuwa ziara hiyo imekuwa ni yenye manufaa kwake na Tanzim kwa ujumla kwani ameweza kujionea hali halisi ya Tanzim ilivyo. Hivyo itamsaidia katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Tanzim kwa ufanisi katika matawi aliyoyatembelea. Anaamini kuwa mipango aliyowapelekea na miongozo aliyowapa iwapo itafanyiwa kazi, italeta mabadiliko makubwa ya kusonga mbele kwa Tanzim, Jamaat na Islam kwa ujumla.

Mwenyezi Mungu Apokee juhudi na maombi yetu katika jambo hili. Na neno langu la mwisho ni kila sifa njema zinamstahiki Allah - Mola wa walimwengu.

Mwisho.

Haki za Wanawake Katika Islam

Kutoka uk. 12

za uzuri wake au ukoo wake, mwanamke aliwahi kumzidi nguvu mwanamume na hata aliwahi kuwa Malkia kama vile wa Sheba, na katika baadhi ya nchi akawa huru kutenda atakavyo, lakini hiyo ilikuwa ni bahati nasibu iliyowaangukia wachache kwani kwa ujumla hakukuwa na sheria maalum iliyolinda haki zao.

Kwenye shimo hilo la kiza, mwanamke hakuwa na haki ya kumiliki chake. Mara aolewapo kila kitu kilikuwa cha mumewe. Hakuwa na haki ya kurithi chochote katika mali ya baba yake, wala kaka yake wala kijana wake zama afarikipo bali hakuwa na haki ya kurithi chochote katika mali za mumewe hata kama wakati wa maisha yao alikuwa akisimamia na kuchangia kwenye uchumaji wa mali hizo.

Mwanamke aolewapo - na wakati mwingi bila ridhaa yake - alikuwa ni kama aliyeuzwa kwa jumla kwa mumewe na wakati ambapo mume alikuwa na haki ya kumuacha au kumtelekeza mkewe wakati wowote bila kuulizwa, mwanamke hakuwa na haki ya kwenda popote nje ya kuta za nyumba ya mumewe wala kudai kuondoka hata kama angekabiliwa na mashaka ya kufa mtu.

Kama mume angemkimbia mke, hakukuwa na sheria yoyote iliyomlinda na ilimbidi ajitafutie maisha yake na pengine ya kuwatunza watoto wake. Mwanamume kwa hasira zake tu, alikuwa na haki ya kumpiga mkewe atakavyo bila kuzuiwa na yeyote na mke hakutakiwa hata kuinua sauti. Kama mume afariki katika baadhi ya nchi na jamii mke alihesabiwa kuwa mali ya jamaa za mumewe ambapo wangeweza kumwoza kwa mtu mwingine wamtakae ama kwa kumgawia kama zawadi au kwa kuchukua cha kwao. Baadhi ya wakati mkuu wa familia ya mume angeweza kuishi na mke wa nduguye aliyefariki bila ridhaa ya mwanamke mwenyewe jambo ambalo liliwapelekea baadhi ya akinamama majasiri waamue kuzikwa au kuchomwa moto wakiwa hai na miili ya waume zao kuliko kulazimishwa kuishi na watu ambao dhamira zao hazijawaridhia.

Si hayo tu bali katika baadhi ya nchi na jamii mwanamke alikuwa ni sehemu ya mali ya mumewe, angeweza kumuuza wakati wa shida, au kumuweka rehani kwa mkopo na ashindwapo kulipa deni angeweza kumtoa mkewe kama fidia, au pengine mume angeweza kumfanya mkewe kuwa mtaji wa kuchezea kamari.

Kwenye kadhia hii ya kutisha, mwanamke hakuwa na haki ya maamuzi juu ya malezi ya watoto wake bali hata uhai wao, kwani vipo visa vya kuzima moyo vya wanaume wababe walioamua kuwazika mabinti wakiwa hai eti kwa sababu walitaka mke wao awazalie kijana lakini akashindwa. Kama mwanamume fulani angeamua kumwacha mkewe angeweza kumuacha njia panda, bila makazi, akiwa hahehohe bila ya kumpatia chochote na watoto wote wangeweza kuchukuliwa



Mtoa mada, Abdulrahman M. Ame, akiwa mbele ya jukwaa wakati akitoa mada yake

na mume bila mama yao kupata haki ya kuwaona tena maishani mwake.

Kwenye upande wa kidini mwanamke ndio hakuwa na chake kabisa. Baadhi ya jamii ziliamini kwamba mwanamke ni mwovu kwa asili ya kuzaliwa, hakuwa na haki ya kushiriki kwenye ibada wala kutoa sadaka kwenye mali yake au kumgawia yeyote ampendaye kama vile ndugu bila ya ridhaa ya mumewe.

Kutoka kwenye shimo hilo Islam ikaja, na mafundisho yake yakawaokoa wanawake mara moja na kuwafungua kwenye minyororo yote kama vile kuvunja kijiti. Kwa hakika Mtukufu Mtume Muhammad s.a.w. alitangaza kwamba moja ya majukumu yake aliyotumwa na Mola Muumba wa walimwenguni kuja kuwakomboa wanawake.

Mafundisho ya Islamu yakatangaza kwa jina la Mungu kwamba wanawake na wanaume kwa kuzingatia asili yao, wote ni sawa na inabidi waishi pamoja kama wenzi au marafiki (4:2, 49:14). Waamuapo kuishi pamoja waelewe kwamba mke anayo majukumu kama vile ambavyo mume anayo majukumu yake na mume anazo haki kama vile mkewe alivyo na haki zake (2:229). Mwanamke anayo haki ya kumiliki mali kama vile mwanamume alivyo na haki hiyo na mume hana haki ya kutumia chochote kutoka kwenye mali ya mkewe bila ya kupewa ruhusa (4:33). Hata kama mke - labda kwa sababu ya kuona haya - aamue kunyamaza kimywa amuonapo mumewe akitumia mali yake bado mume aelewe kwamba iwapo mkewe hayuko radhi na matumizi hayo basi atakuwa amefanya dhambi mbele ya Mwenyezi Mungu. Kama itokezee mume amgawie mkewe kitu chochote basi hatokuwa na haki ya kukinyang'anya tena kutoka kwake.

Mwanamke akatangazwa kuwa na haki ya kurithi mali ya mumewe, baba yake, mama yake, watoto wake na jamaa zake wengine. (4:33-34). Isipokuwa katika mazingira fulani kwa sababu ya majukumu maalum waliyobebeshwa wanaume ya kutafuta matunzo ya kila siku ya familia zao, imefundishwa na Mola mwenye hekima kwamba mwanamke atapata nusu ya kile atakachokipata mwanamume wakati wa kurithi.

Ikafundishwa na Islam kwamba ndoa ni fungamano takatifu ambalo kila mmoja apate nafasi ya kuishi kwa furaha, amani na upendo, lakini hata hivyo ifikiapo mahala ikaonekana kwamba maisha hayawezekani tena kama wawili hao wataendelea na ndoa, basi ruhusa imetolewa kwa wote mke na mume chini ya misingi ya sheria na taratibu zilizowekwa kuachana na mwenzake (2:230 - 233).

Pia imefundishwa kwamba kama itokezee mume kuchukizwa na aamue kujitenga na mkewe basi kujitenga huko hakuwezi kukazidi miezi minne na itambidi mume aamue ama kuafikiana na mkewe au kumpa talaka aende zake (2:227-228). Kama mume ashindwe kumtunza mkewe na aamue kumtelekeza na kumkimbia ndoa yao itahesabiwa kuwa sio ndoa tena baaada ya kupita kipindi fulani. Kwa kuzingatia mazingira mbalimbali wanaulamaa wengi wa Kiislamu wamekubaliana kwamba kipindi cha miaka mitatu kinatosha mno kuifanya ndoa kuwa si ndoa iwapo itajiri hali hii, na mke atakuwa huru kuolewa na mwingine ampendaye.

Mume ametakiwa muda wote atekeleze wajibu wake wa kumtunza mke na watoto (4:25, 4:35). Iwapo atahisi ubaya wowote na aamue kumfunza mkewe nidhamu, basi nidhamu hiyo isifunzwe kwa njia ya adhabu ya kuudhuru mwili, tena awe na ushahidi wa kumtia hatiani mkewe na sio dhana bali wakati mwingi inambidi apate msaada wa kisheria.

Mume katia Islam hajamnunua mke, hana haki ya kumuuza wala hana haki ya kumfanya kuwa mtumishi wa nyumbani. Mke anayo haki kisheria ya kupata matunzo sawa na uwezo wa mumewe. Linahesabiwa kuwa ni kosa kubwa kwa mume kumfanya mkewe aishi chini ya kiwango anachoishi yeye.

Afarikipo mume ndugu zake hawana haki yoyote juu ya mjane na baada ya kipindi kifupi cha eda cha kama miezi minne na siku kumi hivi ili kauangalia haki za kila upande mke anayo haki ya kwenda apendapo na kuolewa na amtakaye (2:235).

Sheria ya Islamu inazidi kufundisha kwamba mbali na sehemu yake maalum ya urithi kisheria, iwapo mume amewacha mali basi mke/mjane apatiwe matunzo ya mwaka mzima ikiwemo kutokutolewa kwenye nyumba ya mumewe kwa kipindi cha mwaka mzima ikiwa kama njia ya kujipanga kiakili na kisaikolojia (2:241).

Kwenye mamuzi ya malezi ya watoto sauti ya mama haiwezi kupuuza itufundishavyo Islam. Kunyonyesha na kuwaangalia watoto wadogo kote kunategema ushauri wake. Ifikiapo kwamba mke na mume hawawezi kuishi tena pamoja na ikabidi waachane, ulezi wa watoto wadogo unakuwa juu ya mama. Bila shaka, wakuapo, kwa sababu za kupata elimu wanatakiwa waende kwa baba yao, lakini muda wote ambao watoto wanaishi na mama yao, gharama za matunzo yao inabidi zitolewe na baba. Katika mazingira hayo, baba pia atalazimika kulipia muda na kazi ambazo mama atafanya kwa ajili ya kuwatunza watoto (2:234).

Kwa ufupi mafunsisho ya Islamu yamefundisha kwamba mwanamke hana daraja ya utegemezi kwa mwanamume, milango yote ya maendeleo ya kiroho iko wazi kwa ajili yake kama ilivyo wazi kwa ajili ya wanaume. Katika maisha yajayo anaweza kupata daraja la malipo mema sawa na malipo awezayo kuyapata mwanamume bali katika maisha ya kidunia anayo haki ya kushika majukumu yoyote katika uongozi na kazi za kijamii kama vile ashikavyo mwanamume na sauti yake inayo nafasi kama sauti ya mwanamume (33:36; 33:74; 4:125) n.k.

Ninaomba nisiishie hotuba yangu bila kutaja kwa kifupi vitu viwili navyo ni hijabu kwa akina mama na ukewenza.

Mwenyezi Mungu ambaye ametuumba wanawake na wanaume kwa lengo maalumu la kumuabudu na kutupa vipaji na uwezo mbalimbali ili tuweze kufikia lengo hilo anatujua sana uimara wetu na udhaifu wetu kwa kila jinsia. Kwa msingi huo ametoa mafundisho ambayo siku zote yanakuza uimara wetu badala ya kuuacha udhaifu wetu utuangamize.

Miongoni mwa sehemu ambayo uimara na udhaifu wa kijinsia unaweza kupimwa vizuri ni kupitia kuijisitiri miili. Kwa kawaida wanawake hawavutwi kwa kiwango kile ambacho wanaume huvutwa waonapo sehemu za mwili wa mwanamke ukiwa wazi. Kwa msingi huo, Islamu kwa ajili ya kulinda heshima ya mwanamke imemfundisha mwanamke wa Kiislamu ajisitiri badala ya kuhemkwa wazi mabarabarani akisubiri kuudhiwa kwa kuitwa hapa na pale na watu wenye uchu iwapo maumbile yake yatawachwa wazi. Sitara itakiwayo ni kujifunika mwili wote kwa kadiri iwezekanavyo. Ni imani yangu kwamba wanawake wenyewe ni mashahidi juu ya ukweli huu kwamba mwanamke aliyejisitiri yuko salama zaidi kunaswa kwenye mitego ya mabweha na mbwa mwitu kuliko mwanamke yule aliyeamuwa mwenyewe kujifanya ulimbo wa kunasia kila kipitacho njiani mithili ya nyumba ya buibui.

Ukeweza katika Islam ni fundisho ambalo limekusudiwa kwa ajili ya makusudi maalum ya kuwa kama 'vali ya usalama' safety valve katika matatizo ya kimaadili na kiutamaduni ambapo bila ya kutoa mwanya huo ni ama jamii itaangukia kwenye maasi ya uhawara na ukahaba au kujidhulumu kwa uruhubani na kuua vipaji. Sote tunaelewa kwamba jamii zilizojifunga kwenye fundisho la mke mmoja tu zimezama kwa kiasi gani kwenye uzinzi, umalaya, mahusiano ya jinsia moja kimapenzi na machafu mengine yasiyofaa kutajwa mbele za watoto na hayo hayaonekani kwao kuwa ni kinyaa.

Bila shaka mke mmoja au wengi sio sababu pekee ya jamii kujizuia na maovu lakini kupitia ruhusa ya wake wengi inapobidi na chini ya masharti kisheria likiwemo lile la uadilifu, shimo lile linakuwa limefunikwa ambalo anayependa kuwa mwema angelitumbukia bila hiyari.

Pia ni vyema akinamama waelewe kwamba lengo la ndoa katika Islamu ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na wala sio kutimiza matamanio ya kimwili hivyo ukewenza umekusudiwa kuwasaidia wao zaidi katika hali za kufiwa na waume, kuachika, kukosa kuolewa kwa muda mrefu n.k. kuliko kuwafungulia wanaume mlango wa kutimiza matamanio yao tu.

Kwa haya machache ninawaomba Lajna Imailla (kinama wa Kiahmadiyya) wajione kuwa ni watu wenye bhati mno kuzaliwa katika zama hizi.

Ndani ya Jamaat Ahmadiyya haki zao zilzioelzwa an Islamu zimelindwa zaidi.

Akinamama wakumbuke kwamba hata ndani ya makundi mengine ya waislamu kwa sababu ya kutokuelewa kwao vizuri mafundisho ya Islamu bado wanawanyima akina mama haki zao.

Mfano" Afghanistan na wanawake kutokupewa haki ya Khulaa.

Redio Iman na wanawake kutokuwaruhusu kuongea n.k.

Lakini ndani ya Jumuiya mmelindiwa haki zenu zote, mmeunidwa umoja wenu, mpewa haki ya kujieleza, haki ya kuchaguana ba kuwekana kwenye uongozi wenu tena bila ya hata Amir wa nchi kukuingilieni kwenye mamuzi zaidi ya kukushaurini. Mnapewa nafasi ya kuongea hata kwenye Shura. Siku hizi kupitia MTA mnaweza kuona na kuwasikia kinamama wakifasiri hotuba za Makahalifa na kushiriki vipindi mbalimbali vya kimaadili na mafunzo.

Hivyo mnayo bahati msiikufuru. Mshukuruni sana Allah na zaidi hayo msiyaonee haya mafundisho yake. Simameni kifua mbele kwa unyenyekevu mkiulekeza ulimwengu kwenye uzuri wa Islamu. Kuweni mashahidi wa ukweli na uzuri wa mafundiaho ya Mola wenu. Mwenyezi Mungu hangeweza kamwe kukudhulumuni, msitahini, muogopeni na mheshimuni. Jalini mafundisho yake, teteeni aliyoyaagiza iwe mnaelewa hekima zake au la. Eleweni kwamba dhamana ya pepo ya dunia na akhera kwa ajili ya familia zenu ipo chini ya maamuzi yenu, Kama mnataka familia zenu na kizazi chenu kikue kiutu na kimaaadili basi kuweni wa Mungu.

Mwenyezi Mungu atuzaidie sote.

Allahumma Rabbanaa hablanaa min azwajinaa wadhuriyyatinaa qurata a'yuni waj'alna lil muttaqiina imaama. Amin.

Khalifa Mtukufu alaani filamu inayokashifu Islam

Kutoka uk. 12

kinyume kabisa na mafundisho ya Islam na kuongeza kwamba kuharibu mali au kuchoma majengo ni vitendo vibaya kabisa na havifaidishi upande wowote, isipokuwa wale ambao wanataka kuchafua jina la Islam.

Akizungumzia suala la uhuru wa kujieleza, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema kwamba watu wanatakiwa kamwe wasione vigumu kukubaliana na ukweli kwamba sheria au kanuni zinazotengenezwa na mwanadamu zinaweza kuwa na dosari au walakini. Alisema kuwa kuchukulia suala la "uhuru wa kujieleza" kama msingi wa kuendeleza amani na maelewano duniani ni dhana potofu.

Akizungumzia kuhusu hitaji la kutoa kipaumbele kwa baadhi ya haki dhidi ya nyingine, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema:
"Amani ya dunia isiharibiwe kwa kisingizio cha uhuru wa kujieleza."

Hadhrat Mirza Masroor a.t.b.a pia aliwataka viongozi duniani na wanajamii kutafakari kama wamechangia katika kusababisha uhasama kwa kuunga mkono, kwa gharama zote, kile kinachoelezwa kuwa ni haki ya watu ya kutengeneza filamu au katuni ambazo zinaudhi na kushambulia dini zingine sanjari na kuwajeruhi watu wasio na hatia.

Katika kujibu uchochezi wa aina hii, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a aliwataka Waislam kote duniani kwa pamoja kuonyesha ukomavu katika kujibu uchochezi huo. Alisema, Serikali za Kiislamu na Waislam wanaoishi katika nchi za Kimagharibi wanatakiwa kuungana ili kutangaza mafundisho ya amani na ya kweli kuhusu Islam na Qur'an Tukufu. Alisema wanatakiwa wawe na msimamo wa pamoja na kwa njia ya amani waitetee Islam na tabia njema za Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w).

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema:

"Waislam wanatakiwa waelewe kwamba kuwa na msimamo mkali sio jibu la uchochezi wa aina hii. Badala yake, wanatakiwa kujirekebisha nafsi na kujibu kashfa za wapinzani kwa kumsalia Mtume Mtukufu (s.a.w). Aidha, ulimwengu wa Kiislam unatakiwa kuungana, na Waislam wanaoishi katika nchi za kimagharibi wanatakiwa kutumia ipasavyo nguvu ya haki yao ya kupiga kura."

Khalifa Mtukufu a.t.b.a alibaini kwamba katika miaka ya hivi karibuni mashambulizi ya aina hii kwa Islam yameongezeka ilhali njia zisizofaa kujibu mashambulizi haya zifanywazo na baadhi ya Waislam zinatakiwa kulaaniwa.

Akizungumzia juhudi za Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya katika kuelezea mafundisho sahihi ya Islam duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema:

"Sisi Waislamu Ahmadiyya tunakuwa mstari wa mbele linapokuja suala la kuhudumia wanadamu. Mathalani, mwaka uliopita, kufuatana na mahitaji makubwa yaliyokuwepo, tulijitolea chupa 12,000 za damu kwa wamarekani na kwa sasa pia tunafanya jitihada kama hizo kujitolea damu. Hivyo, tunajitolea damu katika juhudi za kuokoa maisha, lakini wengine kwa kuunga mkono vitendo viovu na kuchukiza watu, husababisha nyoyo zetu zipate majonzi."

Khalifa Mtukufu V a.t.b.a alihitimisha kwa kuzungumzia kuhusu jinsi majaribio yote yanayofanywa kumdhihaki Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w) kuwa yatashindwa. Alisema:

"Itakumbukwa kwamba Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya, Masihi Aliyeahidiwa (a.s) alisema kwamba kila ushindi unakuja kutoka mbinguni na kwamba Mwenyezi Mungu ameshahukumu kwamba Mtume ambaye dunia inajaribu kumkashifu hatimaye atapata ushindi mkubwa katika dunia hii. Na ushindi huu utapatikana kwa kuzishinda nyoyo za watu."

Katika mkutano huo na Waandishi wa Habari uliofanyika baada ya Sala ya Ijumaa, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a aliwaambia waandishi hao kwamba mapenzi waliyonayo Waislam kwa Mtume Mtukufu Muhammad (Saw) hayana kifani. Alisema kwamba watu wote wanaumia ikiwa wapenzi wao wanadhalilishwa na kwamba shambulio lolote linalofanywa dhidi ya Mtume Mtukufu (s.a.w) kwa hakika linahuzunisha Waislam wote.

Akielezea kuhusiana na maandamano ya vurugu kufuatia kutolewa kwa filamu hiyo, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema kwamba maandamano hayo ni batili na kwamba kuwaua watu wasio na hatia wakiwemo mabalozi na wanadiplomasia ni kinyume kabisa na mafundisho ya Islam. Alisema kwamba maandamano yote yanatakiwa yafanyike kwa kufuata sheria na kwa njia ya amani.

Ijitmai ya Khuddam yafana sana

Kutoka uk. 12

na mafunzo ya dini haswa mafunzo ya jumuiya. Aliwataka Khuddam wote waliohudhuria kwenye Ijitmai hiyo kushiriki katika mashindano mbalimbali ya kimwili na kielimu, akasema lengo la msingi katika mashindano hayo si kupata mshindi, bali ni kupata radhi ya Mwenyezi Mungu.

Alisema makao makuu ya Tanzeem hutuma taarifa nyingi kwenda matawini kwa lengo la kutoa maelekezo na utekelezaji, akasema wakati wa kipindi cha Ijitmai ndio kipindi cha kupima utekelezaji wa maagizo kutoka makao makuu. Aidha Sadr alizungumzia kuahirishwa kwa Shura iliyokuwa ifanyike wakati wa Ijitami hiyo, sadri alisema shura hiyo imeahirishwa kutokana na kutopata kibali kwa wakati, hata hivyo sadri alisema Shura itafanyika wakati wa Jalsa salana ya mwaka huu inshaAllah. Sadri pia alitumia fursa hiyo kumkaribisha rasmi Sadri wa Uganda na ujumbe wake baada ya kutoa pole kwa kusafiri umbali mkubwa ili kuhudhuria na kushiriki Ijitmai ya Tanzania. Alisema hiyo ni ishara ya mapenzi, undugu na kujua haswa umuhimu wa Ijitmai, Sadri alizungumza kwa kifupi juu ya ugeni huo kwa kusema, yeye mwenyewe aliongoza ujumbe uliohudhuria Ijitmai ya Uganda mwaka uliopita. Kwa siku hiyo Sadri wa Uganda alitoa salam tu kwa Khuddam wa Tanzania na kuwatakia Ijitmai Mubarak.

Kama ilivyo ada au majukumu ya Ijitmai, kubwa ni mashindano ya kitaaluma na michezo, Ijumaa kulikuwa na michezo kadhaa iliyoendelea kwa jioni ile, ikiwemo mpira wa miguu nk, wengi walifurahia maana kulikuwa na upinzani mkubwa wa timu zilizoshiriki kwenye mashindano hayo, haswa timu kutoka Jamia "Morogoro", timu ya Dar es Salaam, timu ya Safina na timu ya Ahmadiyya secondary. Hata hivyo timu ya Ahmadiyya secondary waliibuka washindi kwa kuwachapa Ahmadiya Safina mabao 4 kwa 0, hivyo kuwa bingwa wa michuano hiyo kwa mwaka huu.

Jumamosi asubuhi kulikucha na mashindano ya aina mbalimbali yaliendelea, ikiwemo usomaji wa Quran Tukufu, Hadithi za Mtume (saw) hali kadhalika na mashindano ya kimwili ikiwemo michezo ya kuvuta kamba, kutunisha misuli ya mikono nk. Michezo ya kuvuta kamba na kutunisha misuli imeingia kwa mara ya kwanza mwaka huu ambapo ilitia fora sana, wengi waliipenda na kushangilia sana, haswa pambano la utangulizi la kutunisha misuli lililochezwa kati ya Jamil Mwanga na Mwinyimvua Ussi (aliyekaribishwa kama mgeni maalum kutoka Majlis Ansarullah) pambano hili liliwavutia wengi na wengi waliamua kucheza kutokana na utashi mkubwa ulioonyeshwa na watangulizi hao.

Jioni ya siku hiyo kulikuwa na kikao cha pamoja cha Majilis Khuddamul Ahmadiyya ya Tanzinia na Uganda. Masadri wa Tanzania na Uganda, ndio walikuwa wakiongoza kikao hicho, ambacho kimsingi kilikuwa ni kikao cha kubadilishana uzoefu na kushauriana. Mada kuu zilikuwa ni swala la Tabligh, njia gani bora zaidi za kufanya mafunzo ya watoto, swala la utoaji wa michango, majukumu ya Khuddam nk. Hata hivyo ilonekana kuwa kijiografia nchi mbili hizi ziko tofauti sana, kubwa ni kuwa Tanzania ni kubwa kuliko Uganda, hivyo kuna baadhi ya mambo yanaweza kuwa rahisi kwao lakini isiwe rahisi kwa Tanzania, mfano Ijitmai ya Uganda ikiisha



Viongozi wa Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania wakiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi Majlis Khuddamul Ahmadiyya Uganda

tu kuna uwezekano mkubwa wa Khuddam wote waliohudhuria kurudi makwao usiku huo, jambo ambalo si rahisi sana kwa hapa Tanzania, kutokana na hilo, kukawa na wazo kuwa ikibidi, Ijitmai zifanyike kwa kanda, kisha kuwe na moja ya kitaifa itakayojumuisha wajumbe kutoka kanda zote, lengo ni kuhakikisha kila khuddam anapata baraka hii ya Ijitmai, Pia kuliongelewa japo kwa ufupi kutumia fursa zilizopo baina ya nchi mbili hizi kwa kuanzishwa tena kwa jumuiya ya Afrika Mashariki kwa faida yetu pia.

Na kwamba kama Tanzeem, chochote tutakachoona ni muhimu na tunaweza kukifanyia kazi basi hatuna budi kukichukua na kukifanyia kazi kikamilifu, ikiwa ni pamoja na kufanya mawasiliano ya mara kwa mara kati ya Tanzeem hizi. Sadri wa Uganda alisisitiza kuwa ingawa inaonyesha kuwa Tanzania itabadilisha uongozi wa Juu wa Tanzeem sawa na nidham ya Umri ilivyo, lakini Sadri sahib alisisitiza kuwa hata huo uongozi utakaokuja basi hauna budi kuendeleza uhusiano huu muhimu wa kitanzeem na Jumuiya kwa ujumla wake. Kikao hicho kiliendelea mpaka usiku mwingi.

Siku ya Jumapili ilikuwa ni siku ya kufungwa kwa Ijitmai hiyo, siku hiyo ilikuwa na ratiba ndefu, iliyoambatana na utoaji wa zawadi, mkutano na waandishi wa habari, hutuba za viongozi mbalimbali n.k, Sadri sahib wa Tanzania alitoa hotuba fupi ya kumkaribisha Sadri wa Uganda azungumze katika hafla hiyo.

Akizungumza kwa Kiingereza, na hotuba yake kutafsiriwa kwa Kiswahili Sadri huyo wa Uganda alitoa historia fupi ya safari yao ya kuja Tanzania, alisema alituma mualiko mwaka uliopita kwa Sadri sahib wa Tanzania ili kuhudhuria Ijitmai yao (Uganda) iliyofanyika Jinja. Alhamdulillah kwa fadhila za Allah, Tanzania iliweza kushiriki kwa kutuma wajumbe watatu wakiongozwa na Sadri wa Tanzania Mwl. Ally Mbambwa. Mwaka huu aliendelea kusema Sadri Sahib huyo wa Uganda kuwa, alipokea mualiko kutoka kwa Sadri wa Tanzania ili kuja nao kushiriki nasi katika Ijitmai ya hapa Tanzania, Alhamdulillah kwa fadhila za Allah ameweza kuja yeye mwenyewe akiongozana na ujumbe wa watu 7, kama walivyotajwa hapo juu, aliendelea kusema kuwa kuja kwao hapa Tanzania ni sawa tu wako nyumbani, kwani Amir na Mbashiri mkuu wa Tanzania kwa sasa, sheikh Tahir Mahmood Chaudry aliishi Uganda kwa muda mrefu, hivyo ni mtu wanaemfahamu na wamefurahi kukutana naye tena akiwa hapa Tanzania. Alisema sheikh Chaudhy alipokuwa nchini Uganda, waliweza kufungua matawi mengi ya jumuiya, na kuwa kwa jinsi wanavyomfahamu ni mtu mzuri na hivyo tumtumie vizuri haswa katika swala la Tabligh.

Itaendelea, Inshallah

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Dhul-Hijja 1433 AH | November 2012 | Nubuwwat 1391 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin 'Amr bin 'Aas r.a. ya kuwa Mtume s.a.w. alisema: Mwislamu ni yule ambaye Waislamu wengine wanasalimika katika ulimi wake na mkono wake na Muhajir (Mhamaji) ndiye yule ayahamaye Aliyoyakataza Mwenyezi Mungu. (*Bukhari*)

Khalifa Mtukufu alaani filamu inayokashifu Islam

Asema kujibu kwa maandamano ya vurugu, kuchoma ofisi za balozi, kuwaua watu sio mafundisho ya Islam

Na Jamil Mwanga,
Dar es Salaam

Kiongozi wa Jumuiya ya Waislam Ahmadiyya Duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifa wa Tano a.t.b.a amewataka Waislam kote duniani kuungana na kupinga kwa amani filamu iitwayo '*The innocence of Muslims*' ambayo imechochea chuki na hasira miongoni mwa Waislam duniani. Kiongozi huyo ametaka kuwepo na mipaka ya uhuru wa kujieleza ili kulinda hisia za kidini za watu wote.

Katika hotuba yake ya Ijumaa aliyoitoa na kurushwa moja kwa moja kupitia televisheni ya kimataifa ya MTA kutoka msikiti wa Baitul Futuh, London mnamo tarehe 21 Septemba, 2012, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema kwamba Waislam kote duniani wamekerwa na kuumizwa na filamu hiyo sambamba na uamuzi wa gazeti maarufu la kifaransa ambalo kwa mara nyingine tena lilichapisha katuni iliyochorwa kumkashifu Mtume Mtukufu Muhammad (Saw).

Vyombo mbalimbali vya Habari vikiwemo BBC National News, BBC Newsnight, Sky News, Sky Arabic, Reuters walihudhuria mkutano huo na kukutana na Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a muda mfupi tu baada ya hotuba yake ya Ijumaa.

Katika hotuba yake, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alisema kuwa ni kutokana na kuihofia Islam ambako kunasababisha waendelee kutoa video zinazodhalilisha Islam na mashambulio mengine kama hayo dhidi ya Islam.



Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a
Khalifatul Masih V

"Kutokana na kutoweza kwao kuishinda Islam hali inayosababisha wapinzani kukimbilia kufanya vitendo vibaya wanavyojaribu kuvihalalisha kwa kisingizio cha uhuru wa kujieleza", alisema.

Aidha, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a alilaani vurugu zinaoshuhudiwa katika nchi nyingi zikifanywa na Waislam wenye msimamo mkali kwa lengo la kujibu uovu wa filamu hiyo. Alisema kwamba kuwaua watu wasio na hatia wakiwemo mabalozi na wanadiplomasia ni

Endelea uk. 11

Haki za Wanawake Katika Islam

Hotuba iliyotolewa kwenye Mkutano wa Mwaka (Jalsa Salana) Tanzania, iliyofanyika Kitonga, Dar es Salaam 2012

Abdulrahman M. Ame
Dar es Salaam

Enyi watu! kwa hakika Tumewaumbeni katika kiume na kike, na Tumewafanyeni mataifa na makabila ili mjuane; hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye zaidi katika ninyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye habari. (49:14)

Sawa na hekima ya Uumbaji, Mwenyezi Mungu ameumba kike na kiume katika kila kitu, lengo kuu likiwa ni kuufanya ulimwengu wake ubaki katika hali ya utulivu, mafanaikio na kuwa endelevu bali unaowezekana kuishika.

Katika wanadamu pia Mwenyezi Mungu Ametuumba wanawake na wanaume, lakini kama asemavyo katika aya nilizozisoma hivi punde, tofauti hiyo ya maumbile ya kuwa wanawake na wanaume haijakusudiwa kamwe kuonesha kwamba sisi ni viumbe viwili tofauti wala haijakusudiwa kamwe kuonesha ubora wa jinsia moja juu ya nyingine au kuidunisha moja chini ya nyingine. Kinyume chake hiyo ni mipango ya Mwenyezi Mungu ambayo viumbe hatuna mamlaka nayo. Kila jinsia ipo kwa makusudio yake na haja yake maalum. Hakuna jinsia inayoweza kuishi pekee bila kuitegemea nyingine bali hakuna jinsia inayoweza kumea pekee bila ya mwenzake.

Hata hivyo, kwa bahati mbaya mno historia ya mwanadamu imerikodi kumbukumbu chungu ya jinsia moja ya wanadamu - mwanamke - kuonekana kwamba ni kiumbe asiye na hadhi kama ile aliyonayo mwanamume. Hali hii imeendelea kwa kipindi kirefu mno, na bado ipo, ingawaje katika zama zetu za leo kwenye ustaarabu wa Ulaya na Marekani, ambao unaonekana kuwa ndio unaoiendesha dunia yetu, kwa sababu ama ya mwanamke kujikomboa kimabavu kutoka kwenye makucha ya mfumo dume au ya wanaume wenyewe kuchoshwa na utumiaji wa mabavu kijinsia, mwanamke amejiamualia uhuru wake mwenywe, na mambo yameenda kwenye ncha nyingine ya msimamo mkali wa mwanamke kujipa uhuru wa kutenda apendavyo. Uhuru huu - kama hata hivyo unastahili kuitwa uhuru - umewafanya wanawake wengi wa leo wakiwemo baadhi ya Waislamu waone kwamba mwanamke mstaarabu hasa ni yule anayeishi kizungu, anayevaa kimarekani na anayeyeangalia mambo Kiyuropa.

Wako akinamama miongoni mwa Waislamu ambao kwa kuburuzwa na mawazo ya kimagharibi wanadhani kwamba hata sheria za Kiislamu juu ya hijabu (mavazi ya sitara), mirathi, ndoa, majukumu ya malezi ya watoto n.k. yanawaonea, kuwadhalilisha na kuwanyima uhuru na maendeleo yao.

Si ajabu kuwaona baadhi ya akinadada hasa wajidhaniao kwamba ni wasomi - wakiyaonea haya mafundisho ya Kiislamu kuyatekeleza hadharani na mara nyingi wakishindwa hoja za kuyatetea pale yanapolaumiwa na kukebehiwa.

Mada hii kama ilivyosemwa na Mwenyekiti itajaribu kwa ufupi mno kuonesha kwamba kama kuna mafundisho yaliyowaokoa, yaliyowatoa kwenye shimo la kiza na dhuluma na yaliyolinda heshima, haki na uhuru wa mwanamke, basi mafundisho hayo hayawezi kuwa mengine na kwa hakika hakuna mengine zaidi ya mafundisho ya dini Tukufu ya Islamu.

Hata hivyo kabla ya kuyaeleza hayo naomba nikusimulieni wasikilizaji wapendwa sifa za shimo lile ambalo mwanamke wa Kiislamu ameokolewa nalo tena kwa kamba ngumu isiyokatika ili atoke humo.

Kabla ya ujio wa Mtukufu Mtume s.a.w yaani kabla ya ujio wa mafundisho ya Islamu mwanamke, karibu duniani kote, hakuwa zaidi ya mtumwa na chombo cha starehe kwa mwanamume. Hakuna dini iliyomtetea wala ufalme uliomjali na kumlinda. Hata kama tukubali kwamba hapa na pale kwa sababu fulani fulani ama

Endelea uk. 10

Ijitmai ya Khuddam 2012 yafana sana

Na Mwandishi wetu

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, Ijitmai ya Tanzeem ya Khudamul Ahmadiyya ilifanyika tarehe 15 hadi 17 ya mwezi wa Juni 2012 kwa mafanikio makubwa katika viwanja vya Kitonga wilaya ya Ilala nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam. Ijitmai hiyo ambayo ilihudhuriwa na Wanajumuiya hususan Khuddam na Atfal Ahmadiyya zaidi ya 300 kutoka karibu mikoa yote ya Tanzania na wageni kutoka nchini Uganda. Wageni kutoka Uganda walikuwa wanane, waliongozwa na Sadri Sahib Khuddamul Ahmadiyya Uganda ndugu Haroun Mubiru, wengine walioongozana naye kwenye msafara huo ni pamoja na Muhtamim Tabligh & Tarbiyyat ndugu Qassim Kirigwajo, Mu'tamad Bw, Badru Lubowa, Muhtamim Tarbiyyat,Ndugu Siraj Galabuzi, Muhtamim Isha'at, ndugu Abdul Karim Nadooka, Muhtamim Nau Muba'een, ndugu Musa Mubiru, Muhtamim Sihat-e-Jisman, ndugu Yaqoot Nsubuga na ndugu Rajab Kazaan, mwanachama wa Tanzim. Ugeni huo mkubwa ulifika nchini Tanzania siku mbili kabla ya kuanza kwa Ijitmai yetu. Msafara ulipokelewa kituo cha mabasi cha Ubungo na kuanza ratiba yao kama ilivyopangwa.

Siku ya pili wageni hawa walifika msikitini na kuonana na Amir na Mbashir mkuu, pia kuona mazingira kidogo ya msikitini na jiji la Dar es Salaam kwa ujumla. Haikuwa ziara maalum lakini walau waliweza kuona bahari ya Hindi, bandari ya salama, ikulu na hospital ya saratani ya Ocean Road. Jioni ya siku hiyo hiyo tulishiriki nao kwenye mazishi ya Mwl Labandin Amani katika eneo letu la Temeke, Dar es salaam (***Inna lillahi wainna ilaihi raaji'uun***), Kisha wageni wetu walielekea eneo la kitonga tayari kwa kuanza kwa Ijitmai siku iliyofuata.

Kama kawaida, Ijitmai ilifunguliwa baada ya swala ya Ijumaa iliyoongozwa na Mwl. Abdulrahman Ame, Kisha kikao cha kwanza kilianza na mgeni rasmi alikuwa ni Sadri wa Tanzania Mwl. Ally Hamisi Mbambwa. Akizungumza katika ufunguzi wa Ijtmai hiyo, Sadri Sahib wa Tanzania Mwl. Ally Mbambwa alizungumzia umuhimu wa Khuddam kujitolea na kufanya kazi za jumuiya kwa bidii kubwa, alisisitiza swala la kufanya ibada na kushikamana

Endelea uk. 11